

**FLICK APONGEZWA KUWAJENGA CHIPUKIZI**

UKURASA 22

**VIASHIRIA** ugaidi, uhalifu mtandao kikwazo usalama Afrika Mashariki



UKURASA 2

**UTOAJI** hati miliki ardhi watolewa kwa saa 24

UKURASA 4

**WENYE** ulemavu waonywa kuhusu ulaghai kukubali mila potofu

UKURASA 5

epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Jumamosi Oktoba 26, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581841

www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US 0745 700 710 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital

## KESI MAUAJI ASIMWE

# Padri aanza kujitetea

**ADAI** kuwa na matatizo ya kusahau, Jaji aamuru apimwe akili...

*Endelea Ukurasa wa 3*



Waombaji, Bob Chacha Wangwe (wa pili kulia), Ananilea Nkya (kushoto), wakijadiliana jambo na mawakili wao, Mpale Mpoki (wa tatu kulia) na Jebra Kambole (wa pili kushoto), katika chumba cha Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana, baada ya kuahirishwa kwa kesi ya kuitaka Mahakama iondoe mamlaka ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa hadi Oktoba 28, mwaka huu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# CHADEMA yapinga takwimu uandikishaji uchaguzi wa S/mitaa

UKURASA 3



## Mtanzania achaguliwa ukurugenzi Benki ya Dunia

UKURASA 4

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba (kulia), akimpongeza Dk. Zarau Kibwe kwa kuchaguliwa na Benki ya Dunia kuwa Mkurugenzi Mtendaji mpya wa benki hiyo atakayesimamia Kanda Namba Moja ya Afrika, inayojumuisha nchi 22 ikiwamo Tanzania, wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Benki ya Dunia wa Kanda Namba Moja ya Afrika, uliofanyika jijini Washington D.C, Marekani. **PICHA: WF**

**MICHEZO** **SIMBA SC YAENDELEZA DOZI** UK. 24 **KATUNI** UK. 6

# Mamalishe kicheko kupaa bei ya korosho

**Na Baraka Jamali,** MTWARA

MAMA ntilie wanaouza chakula katika maeneo mbalimbali mjini hapa, wameeleza kufurahishwa kuanza kwa msimu mpya wa korosho baada ya kuwapo kwa neema kwao kutokana na kupanda kwa bei ya zao hilo.

Wamesema kupanda kwa bei ya zao hilo, kumewafanya wao pia kuneemeka kiuchumi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na mwandishi wa habari hii, baadhi ya mamalishe walisema tangu kuanza kuuzwa kwa korosho, biashara yao imeimarika na wateja wameongezeka.

"Awali nilikuwa napika kilo mbili za unga kwa ajili ya chapati, lakini sasa na pika kilo tatu na nusu kila asubuhi," alisema Chepi Salum na kuongeza kuwa hali hiyo imemwezesha kumudu ada ya shule ya mwanawe.

"Sasa sihangaiki na fedha za ada na kila nikipata ninampelekea mwanangu," alisema huku akionyesha tabasamu usoni mwake.

Mwanahamisi Ibrahim, mamalishe mwingine, alisema kupaa kwa bei hiyo ya korosho kumeleta matumaini makubwa kwa kipato chake.

"Tunatarajia kujenga nyumba nzuri mwaka huu kutokana na bei kuimarika, wafanyabiashara wa chakula tunatumia fursa hii kuboresha maisha yetu. Biashara yetu inategemea wateja wengi wanaokuja kutafuta chakula na tunaweza kujipatia kipato kizuri," alisema.

"Kwa sasa, tunanufaika sana na juhudi zetu na kila mtu anajaribu kufanya vizuri. Bei zimepanda, hivyo tunashukuru kwamba tunapata wateja wengi," alisema Jasmin Owen, mmoja wa mamalishe hao.

Wakati mamalishe hao wakiwa na furaha, wafanyabiashara wengine walilalamikia kupanda kwa bei za bidhaa, wakisema kwamba hali hiyo inasababishwa na gharama za usafirishaji.

Jamiri Hussein, mfanyabiashara wa Soko Kuu la Mtwara, alisema mfumuko wa bei unatokana na gharama za usafirishaji ambao umesababisha ngano na bidhaa zingine bei kuwa juu.

Mfumo wa Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) unawawezesha kuondokana na changamoto za zamani. Karim Sadiki, mkulima wa korosho kutoka Newala, alisema: "Mwaka huu neema iko upande wetu. Tumepata fedha zetu kwa wakati."

Sadiki aliongeza kuwa wanajipanga kufanya maajabu kupitia mauzo ya korosho mwaka huu.

"Hatujui maisha magumu, tumejipanga vizuri," alisema kwa kujiamini.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TMX, Godfrey Malekano, alithibitisha kwamba mkoa wa Mtwara umeleta tani 21,937 za korosho sokoni.

"Bei nzuri inategemea ubora wa bidhaa zetu. Wakati msimu wa korosho unavyoendelea, kinamama na wakulima wa Mtwara wana matumaini makubwa ya kuboresha maisha yao kupitia biashara na kilimo cha korosho.

"Kwa hakika, msimu huu unaonekana kuwa wa matumaini kwa jamii ya Mtwara, huku biashara ya chakula ikichangia katika ukuaji wa uchumi wa eneo hili. Hii ni fursa inayoweza kuleta maendeleo kwa jamii nzima na kuwasaidia wengi katika kujenga maisha bora," alisema.




Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Dk. Shaibu Hamis Kaduara (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Teknolojia za Nishati Jadidifu na Mbadala (REA), Mhandisi Advera Mwijage, wakati wa kufunga Mkutano wa 10 wa Jotoardhi Afrika, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Viashiria ugaidi, uhalifu wa mtandaoni kikwazo usalama

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Kamishna (CP) Ramadhani Kingai, amesema uhalifu ambao bado kikwazo kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni wa mitandaoni na viashiria vya ugaidi.

Amesema kwa upande wa Tanzania, hakuna matukio makubwa ya kimtandao bali yale ya watu aliowaita 'wahuni' wanaobahatisha ambao huandika ujumbe usemao, 'tuma kwenye namba hii' na kwamba operesheni nyingi za kuwakamata hufanyika na kufikishwa mahakamani.

Kingai aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam kwa niaba ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Camilus Wambura, wakati wa mahojiano na waandishi wa habari katika Mkutano Maalum wa Nane wa Wakuu wa Polisi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Alisema pamoja na kuwapo kwa uhalifu huo katika jumuiya hiyo, ziko juhudi za wakuu wa nchi husika na wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama za kushirikiana ili wahusika wasipate muda wa kujipanga na kufanya uhalifu.

"Ninaamini namna wanavyopanga mambo yao kama mikutano hii inavyoelekeza, tumejikuta kwenye nafasi nzuri ya kuhudumia wananchi katika maeneo haya na kuwa salama," alisema.

Kamishna Kingai alisema mkutano huo ni wa nane na umewakutanisha kujadili mambo mbalimbali ya kiusalama hasa uhalifu unaovuka mipaka ikiwamo biashara ya usafirishaji binadamu.

Alisema wamekutana kujadili mambo yaliyoazimiwa mwaka jana na yalivyoshughulikiwa na kuangalia sera zinazohusiana na kazi za polisi kwenye jumuiya hiyo.

"Tanzania ni mwenyeji wa mkutano huu, hivyo tumeshirikiana na taasisi nyingine za haki jinai kama Magereza na Uhamiaji kwa sababu kazi zetu ni moja zinafanana.

"Tumekutana nchi sita za Afrika Mashariki kuhakikisha ardhi ya Afrika Mashariki inakuwa salama kwenye mambo hayo," alisema.

Kingai alisema hali kwa ujumla kwa sasa ni nzuri kwa sababu wanashirikiana kwa kupeana taarifa kati ya nchi na nchi au idara nyingine husika.

Kadhalika, alisema wamekuwa wakibadilishana uzoefu wa maeneo waliyofanikiwa ili kuhakikisha wahalifu hawajitanui, wanawashughulikia kadiri inavyopaswa na nchi zibaki salama.

"Tanzania tuko salama ndiyo maana wenzetu wametuchagua. Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kuendelea kuratibu nchi yetu kwenye eneo hili la usalama. Tungekuwa na vurugu sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki isingeamua kuichagua Tanzania kuwa sehemu ya mkutano huu kufanyika," alisema.

DCI Kingai alisema mambo ya kuzingatiwa ni kuboresha zaidi ushirikiano kwa kushirikishana taarifa.

"Zamani kulikuwa na shida kidogo ya mtu kutoa taarifa zinazohusiana na uhalifu ilionekana ni kutoa siri, lakini kwenye uhalifu unaovuka mipaka huwezi kujifungia na kupata mwenyewe suluhu ya uhalifu uliotokea ni mpaka uende kwa wenzako.

"Mfano uhalifu wa makosa ya kimtandao, mtu yupo nyumbani anaiba benki, zamani ilikuwa wanakwenda na mtutu benki na wananchi wanawekwa chini ya ulinzi na kuiba, sasa hivi anakuwa na simu anaiba benki akiwa nje ya nchi," alisema.

Kingai alisema uhalifu huo ili kuumudu ni kwa kupeana taarifa pamoja na kujengeana uwezo na kujifunza mbinu mpya za kukabiliana nao.

Katika hotuba yake ndani ya mkutano huo, alisema mkutano huo ni fursa nzuri kujadili na kupitisha sera na mipango ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto za kisasa za amani na usalama.

"Kuibuka na kuongezeka kwa matishio ya amani na usalama, kuanzia uhalifu wa kitaifa, uhalifu wa kuvuka mipaka, ugaidi, biashara ya binadamu na dawa za kulevya, vurugu baina ya jamii, mivutano ya kisiasa na kiusalama katika maeneo mbalimbali.

"Ni tishio kwa maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi katika Afrika Mashariki, hivyo basi, kuna haja ya kuandaa mikakati madhubuti ya kupambana na uhalifu wa kisasa katika eneo hili," alisema.

Mwenyekiti wa mkutano huo, Naibu IGP wa Sudan Kusini, Luteni Jenerali Thomas Jal Thomas, aliyemwakilisha Mkuu wa Jeshi la Polisi la nchi hiyo, alisema wako hapa tangu Jumatatu kwa lengo la kuangalia namna ya kukabiliana na uhalifu unaovuka mipaka na kitakachojadiliwa, kitawasilishwa kwa wakuu wao.

KESI MAUAJI YA ASIMWE

# Padri aanza kujitetea, adai ana matatizo ya kusahau

**Na Restuta Damian,**
BUKOBA

MSHTAKIWA namba moja katika kesi ya mauaji ya mtoto mwenye ualbino Asimwe Novert, Padre Elpidius Rwegoshora, jana alianza kujitetea na kudai kuwa ana matatizo ya kusahau.

Hatua hiyo ilisababisha Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Bukoba, Emmanuel Ngogwana, anayesikiliza kesi hiyo, kusitisha mwenendo wa kesi hiyo kwa siku 42 ili apelekwe katika Taasisi ya Akili Isanga kwa ajili ya kufanyiwa vipimo vya afya ya akili.

Jaji Ngogwana alitoa uamuzi huo jana wakati kesi namba 25513/2024 inayowakabili washtakiwa tisa, akiwamo padre huyo ilipofikishwa kwa mara ya kwanza katika Mahakama Kuu Kanda ya Bukoba.

Awali, akimwakilisha mshtakiwa huyo pamoja na wenzake wanane mahakamani hapo, Wakili Projestus Mlokozi aliyeteuliwa na serikali kuwa mtetezi wa washtakiwa hao, aliomba kusitishwa kwa muda uendeshaji wa kesi hiyo ili mahakama itoe kibali kwa mujibu wa sheria, dhidi ya mtuhumiwa huyo kwenda hospitalini kuangaliwa afya ya akili, kwa kuwa wakati akifanya mazungumzo alionekana kuwa ana tatizo.

Hoja hiyo iliungwa mkono na mawakili wenzake wawili upande wa utetezi, kisha Jaji Ngingwana alipoanza kumhoji kwa maswali ya uelewa, aliridhia mtuhumiwa huyo kuchunguzwa akili.

Mahojiano kati ya Jaji Ngogwana na Padri Rwegoshora yalikuwa kama ifuatavyo;-

**Jaji:** Kwa nini upo mahakamani?

**Padri:** Niliambiwa na Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Kagera kuwa niliua mtoto.

**Jaji:** Tangu umezaliwa uliwahi kuwa na tatizo la afya upande wa akili?

**Padri:** Nina tatizo la kusahau na nilisimamishwa kazi kutokana na tatizo hilo.

Baada ya mahojiano hayo, Jaji Ngongwana alisema mahakama haiwezi kuendelea na washtakiwa wengine wanane wanaohusika na kesi hiyo mpaka Padri Rwegoshora atakapofanyiwa uchunguzi.

Jaji aliahirisha kesi hiyo hadi Desemba 11, mwaka huu, itakapotajwa baada ya uchunguzi wa hospitali kukamilika.

Mei 30, mwaka huu, Asimwe alichukuliwa nyumbani kwao, Kata ya Kamachumu, Muleba, mkoani Kagera na Juni 17, mwaka huu, alikutwa kwenye karavati akiwa ameuawa huku baadhi ya viungo vyake vikiwa vimeondolewa.



Sajini Aman Hassan wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Kinondoni, akitoa mafunzo kwa vitendo ya kinga na uokoaji dhidi ya majanga ya moto kwa wafanyakazi wa Kampuni ya The Guardian Limited (TGL) inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, katika ofisi za TGL Mikocheni, Dar es Salaam juzi. **PICHA: MARY KADOKE**

# CHADEMA yapinga takwimu uandikishaji uchaguzi mitaa

**Na Vitus Audax, MWANZA**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Ziwa kimepinga takwimu zilizotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, kwa mikoa ya Kanda za Victoria na Serengeti kwamba hazina ukweli na haziendani na idadi ya watu walioandikishwa.

Katibu wa CHADEMA Kanda ya Victoria, Zacharia Obadi, aliyasema hayo jana mkoani hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu takwimu hizo.

Alisema orodha iliyotolewa TAMISEMI imeitaja Mwanza kuwa ni miongoni mwa mikoa iliyofanya vizuri, jambo ambalo amedai si kweli.

Obadi alisema baadhi ya wilaya za mkoa huo, zilikuwa na idadi ya watu tofauti na wale ambao walikuwa katika orodha wakati mchakato huo unafungwa.

Alisema wamebaini katika mkoa huo kuwapo kwa upungufu katika jimbo la Magu, Kata ya Kisesa, Kijiji cha Wita, Kitongoji cha Igeye, ambako mpaka mchakato huo unafungwa, walioandikishwa ni 823 na orodha iliyobandikwa ilikuwa na watu 1,400, sawa na ongezeko la watu 577.

Katika Wilaya ya Ilemela, Kata ya Kitangili, Mtaa wa Kiloleni, kituo cha eneo la Wazi, mchakato wa uandikishaji ulifungwa kukiwa na watu 674 lakini majina yaliyobandikwa ni 1,131, sawa na ongezeko la watu 457.

"Katika Jimbo la Geita Mjini, Kata ya Mtakuja, Kijiji cha Kampaundi, Kitongoji cha Nyamalembo mpaka mchakato wa uandikishaji unafungwa walioandikishwa ni 355 lakini orodha iliyobandikwa ilikuwa na majina ya watu 892, sawa na ongezeko la watu 537," alisema.

Obadi pia alisema katika jimbo la Bukombe, Kata ya Busonzo, Kijiji cha Nyakanyenze, Kitongoji cha Kawiwizi walioandikishwa ni 91, lakini orodha iliyobandikwa ni ya watu 417, sawa na ongezeko la watu 326.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Simiyu, Mussa Onesmo, alidai kuwa baadhi ya mitaa imeongezewa majina ya wapigakura kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mtaa, kinyume cha utaratibu uliokuwa ukitumiwa wakati wa uandikishaji, hivyo hawako tayari kuona majina yaliyoongezwa yakihusishwa katika upigaji wa kura. Alitaja baadhi vituo anavyodai vimeongezewa majina kuwa ni mitaa ya Nyakabindi, Gagabali, Muungano, Mwahnunda, Guya, Nghesha katika majimbo ya Bariadi Mjini na Vijijini.

Akijibu madai hayo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Adrian Jungu, alisema kanuni inaruhusu kuweka pingamizi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Ngazi ya Kata ikiwa mwananchi hajaridhishwa na shauri litafanyiwa kazi ndani ya siku mbili na kutaka wasilalamike pembeni.

# Wafanyakazi TGL wapatiwa mafunzo majanga ya moto

**Na Mary Kadoke**

JESHI la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Kinondoni, Dar es Salaam limetoa mafunzo ya uokoaji kwa baadhi ya wafanyakazi wa kampuni ya The Guardian Limited (TGL).

Mafunzo hayo yalitolewa hivi karibuni na Ofisa Habari Uhusiano kwa Umma wa Jeshi hilo, Sajini Aman Hassan, kujenga uwezo wa nadharia na vitendo kuhusu kinga na uokoaji wanapopata majanga ya moto.

Katika mafunzo hayo, wafanyakazi walijifunza mbinu mbalimbali za kukabiliana na majanga ya moto ikiwamo matumizi sahihi ya vifaa vya kuzima moto na mbinu za kujiokoa.

"Mafunzo haya yanalenga kuimarisha usalama kazini na kuongeza uelewa wa namna ya kuchukua hatua za haraka na sahihi pindi hatari ya moto inapotokea ili kupunguza madhara na kuokoa maisha na mali katika mazingira ya kazi," alisema.

Sajin Hassan aliwahimiza wafanyakazi kuendelea kufanya mazoezi mara kwa mara na kuhakikisha vifaa vya kuzima moto viko katika hali nzuri na vinapatikana kwa urahisi.

Barasubramaniyan Venkadachalam, Meneja Uchapaji wa TGL, alisema mafunzo hayo yanayotolewa kila mwaka ni sehemu muhimu ya kuimarisha uelewa na ujuzi wa wafanyakazi na jamii kwa ujumla katika kujilinda dhidi ya majanga ya moto.

"Mafunzo ya kinga na uokoaji yanatukumbusha washiriki kuhusu mbinu bora za kuzuia na kukabiliana na moto unapozuka ikiwa ni pamoja na matumizi sahihi ya vifaa vya kuzimia moto, mbinu za uokoaji wa haraka na taratibu za usalama.

"Kwa kujifunza mbinu hizi mara kwa mara, jamii inakuwa tayari kukabiliana na hatari zinazoweza kujitokeza, hivyo kupunguza madhara na hasara zinazosababishwa na moto," alisema.

Philipo Ernest, mmoja wa wafanyakazi wa TGL, alisema mafunzo hayo yamehusisha maelekezo ya kina kuhusu matumizi salama ya gesi nyumbani ili kujikinga na majanga ya moto.

"Washiriki wamefundishwa jinsi ya kuhakikisha vifaa vya gesi vinakuwa katika hali nzuri ya usalama, ikiwa ni pamoja na kukagua bomba la gesi na valvu mara kwa mara ili kugundua uwezekano wa kuvuja kwa gesi. Pia, wamepata maelezo ya kutosha kuhusu umuhimu wa kuweka vifaa vya kuzimia moto karibu na maeneo ya matumizi ya gesi na jinsi ya kuzitumia iwapo moto utatokea," alisema.

# Mtanzania akwaa ukurugenzi Benki ya Dunia

**Na Benny Mwaipaja,**
WASHINGTON DC

BENKI ya Dunia (WB) imemchagua Dk. Zarau Kibwe, raia wa Tanzania, kuwa Mkurugenzi Mtendaji mpya wa benki hiyo atakayesimamia Kanda Namba Moja ya Afrika inayojumuisha nchi 22 ikiwamo Tanzania.

Dk. Kibwe anakuwa Mtanzania wa pili kushika nafasi hiyo kutoka Tanzania. Mtanzania wa kwanza kuhudumu katika nafasi hiyo alikuwa Christopher Kahag, mwaka 1968 hadi 1970.

Uteuzi wa Dk. Kibwe katika nafasi hiyo nyeti kwenye taasisi hiyo kubwa ya fedha duniani, umetangazwa katika Mkutano wa Mwaka wa Kundi la Kwanza la Nchi za Afrika wa Benki ya Dunia, uliofanyika jijini Washington D.C, Marekani ambako Mikutano ya Mwaka ya Shirika la Fedha Duniani IMF na Benki ya Dunia inafanyika.

Kabla ya kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji mpya wa benki hiyo, Dk. Kibwe alihudumu katika Ofisi hiyo ya Bodi kama Naibu Mkurugenzi Mtendaji, Mshauri na Mshauri Mwandamizi kwa zaidi ya miaka saba, tangu mwaka 2017.

Akizungumza jijini Washington D.C, baada ya kutangazwa kuchukua nafasi hiyo, Dk. Kibwe alisema ataitumia nafasi hiyo kusimamia uendeshaji wa benki na taasisi zake pamoja na kutetea maslahi ya nchi katika Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Dunia na maslahi ya Kanda ya Afrika anayoisimamia ili kukuza maendeleo na uchumi wa nchi hizo.

Akizungumza kwa niaba ya serikali katika mkutano huo uliomtangaza Dk. Kibwe kuchukua nafasi hiyo, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, anayeongoza ujumbe wa Tanzania katika mikutano hiyo ya mwaka ya IMF na Benki ya Dunia, alisema hayo ni matokeo ya juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan, kuifungua nchi na kukuza diplomasia ya kimataifa.

Dk. Nchemba alimpongeza Dk. Kibwe kwa kupata nafasi hiyo na kwamba kutokana na umahili wake katika masuala ya uchumi na fedha, pamoja na uzoefu wake wa muda mrefu katika ofisi hiyo, anaamini kuwa maslahi ya nchi yataendelea kulindwa ipasavyo kwa manufaa ya Watanzania.

Dk. Kibwe ni mchumi na kwa nafasi hiyo atakuwa mkurugenzi mtendaji wa kanda inayojumuisha nchi za Botswana, Burundi, Eritrea, Eswatini, Ethiopia, Gambia, Kenya, Lesotho, Liberia, Malawi, Msumbiji, Namibia, Rwanda, Shelisheli, Sierra Leone, Somalia, Sudan Kusini, Sudan, Tanzania, Uganda, Zambia, na Zimbabwe.

Kabla ya kujiunga na Ofisi ya Bodi, Dk. Kibwe alihudumu kama Mchumi wa Benki ya Dunia kwa Tanzania.

Katika kipindi cha miaka 15 ya kazi yake, Dk. Kibwe alihudumu katika Serikali ya Jamhuri wa Muungano katika nafasi mbalimbali ikiwamo ya Mchambuzi Mwandamizi wa Sera katika Ofisi ya Rais - Tume ya Mipango, Mhadhiri Msaidizi (Chuo Kikuu Dodoma), Ofisa Forodha Msaidizi (Mamlaka ya Mapato Tanzania) na Mhadhiri Msaidizi Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere.

Dk. Kibwe ana Shahada ya Uzamivu (Ph.D.) katika Uchumi wa Maendeleo, Shahada ya Uzamili (MA) katika Uchumi wa Maendeleo na Shahada ya Umahiri katika Sera za Umma, zote kutoka Taasisi ya Taifa ya Mafunzo ya Sera (GRIPS) Tokyo, Japan.

Alipata Shahada ya Kwanza ya Sayansi katika Uchumi kutoka Chuo Kikuu Mzumbe kilichoko Morogoro, Tanzania.



Dereva wa bodaboda (kulia), akibandikiwa stika yenye ujumbe wa kuhamasisha kupiga vita dhidi ya rushwa ya ngono, wakati wa kampeni ya Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana, inayoendeshwa na Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), eneo la Mbagala Rangi Tatu, Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Hati za viwanja zatolewa saa 24 wizarani

**Na Joseph Mwendapole**

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imeanza kufanya kazi usiku na mchana kutatua migogoro ya ardhi na kutoa hati za viwanja.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Antony Sanga, alisema juzi wakati akizungumza na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ambaye yuko kwenye ziara za usiku kukagua miradi.

Sanga alisema utaratibu wa kufanya kazi usiku na mchana umekuwa na manufaa makubwa kwa kuwa wamefanikiwa kutatua migogoro mingi na kwa muda huo wametoa hati 7,510.

Alisema walibaini kuwa wakati wa mchana kunakuwa na mrundikano wa watu wanaofika wizarani kupata huduma mbalimbali hali ambayo iliwalazimu kuanza kufanya kazi nyakati za usiku.

"Kuna watu hawana muda wa kuja mchana kwa hiyo usiku inakuwa nafasi yao kupata huduma na huduma hii si kwamba inapatikana hapa wizarani tu bali hata kwenye Manispaa za Kinondoni, Temeke, Jiji la Dasr es Salaam (Ilala), Ubungo na Temeke wote wanatoa huduma za usiku," alisema.

Alisema baadhi ya wafanyakazi wa wizara hiyo wamekuwa wakiingia kazini kuanzia saa 9:00 mchana na kumaliza kazi saa sita usiku baada ya kuonana na kusikiliza changamoto za wananchi.

Alhaji Ali Momba, ambaye alipata hati juzi usiku wizarani hapo, alisema baada ya kusikia huduma hizo zinapatikana usiku aliona ni bora aendelee na shughuli zake mchana ili aje usiku na alikiri kuwa ni kweli alipokelewa na kupata huduma ndani ya muda mfupi.

"Utaratibu huu usiwe wa mpito, uwe wa kudumu ila waongeze mashine za kutolea huduma ila naishukuru wizara kwa ubunifu huu kwa sababu unaondoa usumbufu wa watu kukaa hapa muda mrefu, kuna wakati mtu anakaa hapa siku nzima," alisema.

Mwingine aliyepewa hati ya ardhi usiku, Rehema Buguni, alisema huduma ya usiku imekuwa na manufaa makubwa kwani wakati wa mchana kunakuwa na idadi kubwa ya watu na wanatumia muda mwingi sana kufuatilia masuala ya ardhi. Akizungumza kwenye tukio hilo, Chalamila alisema anashukuru kuona Mkoa wa Dar es Salaam umepewa makamishna wa ardhi wawili kutokana na ukubwa wa mkoa huo.

Alimshukuru Mhandisi Sanga kwa ubunifu huo ambao alisema utaondoa usumbufu wa foleni kwa wananchi wengi wanaokuja kutafuta suluhu ya matatizo ya migogoro ya ardhi.

Alisema wananchi wengi wanasumbuka sana na migogoro ya ardhi kutokana na tabia ya baadhi ya watu kughushi hati za viwanja na mashamba na kuviuza hali ambayo imesababisha mitafaruku.

"Nakushukuru sana Katibu Mkuu kwa sababu mmekuwa wasikivu sana mmetatua migogoro mingi sana ya ardhi na wananchi hapa wametoa mapendekezo kwamba mashine za kutolea hati ni chache kwa hiyo wizara itafute namna ya kuziongeza ili kuhudumia wananchi kwa haraka zaidi," alisema.

Chalamila alisema Mkoa wa Dar es Salaam umeweka azma ya kuhakikisha biashara zote zinafanyika kwa saa 24 hivyo kuanza kwa huduma hiyo ya usiku ni kuunga mkono azma hiyo.

# TMA yakabidhiwa rada mbili zilizokarabatiwa

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imekabidhiwa rasmi rada zake mbili za hali ya hewa zilizoko Mwanza na Dar es Salaam, zilizokuwa zinafanyiwa maboresho na Kampuni ya Enterprises Electronic Corporation (EEC) ya Marekani.

Maboresho hayo yamefanywa na Serikali ya Tanzania kupitia bajeti ya maendeleo yakilenga kuboresha ufanisi wa rada hizo zilizokwishatumika kwa zaidi ya miaka 10 kwa kutoa vifaa vyenye teknolojia yenye kizamani na kufunga ya kisasa ili kupata picha nzuri itakayoweza kutafsiriwa kiurahisi.

Katika makabidhiano hayo yaliyofanyika katika ofisi za rada ya Dar es Salaam, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu TMA ambaye ni Kaimu Mkurugenzi wa TMA, ofisi ya Zanzibar, Masoud Faki, alisema amefuatilia kwa karibu mwonekano wa picha za rada ya Bangulo, Dar es Salaam na ameridhishwa kwa maboresho ya vifaa vilivyohuishwa na kufanya kuwa na uwezo mzuri wa kuona matukio ya hali mbaya ya hewa.

"Kwa kweli nimeridhishwa na namna hivi vifaa vimewekwa na kuona sasa rada zinaweza kufanya kazi kwa kupata picha zenye mwonekano mzuri hadi baharini, hivyo tunatarajia zitatusaidia katika kutabiri hali mbaya ya hewa ili kuokoa jamii dhidi ya majanga," alisema Faki.

Aidha, aliishukuru serikali kwa kuendelea na uboreshaji wa miundombinu ya hali ya hewa ikiwamo ununuaji na ufungwaji wa rada tatu katika mikoa ya Mtwara, Kigoma na Mbeya na kufanya kuwa na jumla ya rada tano mpaka sasa ikiwa ni matazamio ya kufikia mtandao wa rada saba nchini.

Mwakilishi wa EEC Tanzania ambaye, Edwin Kasanga, wakati akikabidhi rada hizo, alisema jukumu la kuziboresha rada hizo kwa kuzifanya ziwe za kisasa na zenye ufanisi mzuri, kwa Mwanza walikamilisha Julai wakati Dar es Salaam wamekamilisha mwezi huu.

Aidha, Kasanga aliwaomba wahandisi wa TMA kuitumia elimu waliyoipokea Marekani kupitia mafunzo ya kujengewa uwezo na watengenezaji, watazitumia vizuri rada hizo ipasavyo pamoja na kuzingatia matumizi sahihi ya programu za kisasa.

Rada hizo zina uwezo wa kufuatilia matukio ya hali ya hewa kwa umbali wa nusu kipenyo cha zaidi ya kilometa 250.

# Ujumuishaji jinsia katika usimamizi rasilimali tatizo

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imesema bado kuna changamoto za kutekeleza ujumuishwaji wa jinsia katika usimamizi wa rasilimaliwatu hali inayosababisha kukosekana kwa uwiano sawa kati ya wanaume na wanawake katika baadhi ya maeneo.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe Juma, alisema hayo wakati akifungua kongamano la nne la wanawake katika uongozi lililoandaliwa na Taasisi ya Uongozi.

"Hali hii inasababisha kukosekana kwa vipaji, mawazo na ujuzi ambao ungeweza kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji wa huduma bora kwa umma," alisema.

Alisema serikali inatambua uzingatiaji wa masuala ya jinsia una mchango mkubwa katika kukuza ustawi wa wananchi na maendeleo ya taifa. Waziri alisema kwa kutambua jambo hilo msisitizo mkubwa umewekwa kukuza usawa wa kijinsia kwenye kufanya maamuzi katika ngazi zote ikiwamo wizara, idara zinazojitegemea, wakala wa serikali, taasisi za umma na binafsi, asasi za kiraia na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

"Ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi na uongozi ni moja ya vipaumbele vya serikali katika kuhakikisha usawa kati ya wanaume na wanawake," alisema.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa wanawake katika nafasi za uongozi wakiwamo, mawaziri, naibu mawaziri, makatibu wakuu, naibu makatibu wakuu na wakurugenzi katika taasisi mbalimbali za umma ni asilimia 28.6 ya viongozi wote.

Waziri alisema hicho ni kiashiria chanya kufikia asilimia 30 ya uwakilishi wa wanawake katika uongozi ambayo ni hatua muhimu kufikia lengo namba tano la usawa wa kijinsia (SDG 5) la asilimia 50 ifikapo mwaka 2030.

Aidha, alisema amefurahi kuona jitihada za Taasisi ya Uongozi katika kuwawezesha viongozi wanawake ili kuondokana na changamoto hizo na mada iliyochaguliwa ya umuhimu wa uongozi wa mabadiliko kwa viongozi wanawake barani Afrika imekuja wakati mwafaka na inafaa katika muktadha wa bara la Afrika.

Alisema mjadala huo utachambua kwa kina sifa mahususi za uongozi wa mabadiliko na manufaa yake na kubainisha changamoto zinazoweza kuwakwamisha na njia bora za kuwavusha kufikia uongozi wa mabadiliko.

Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi, Kadari Singo, alisema wana kongamano la kikanda linalohusisha nchi mbalimbali za Afrika lengo ni kuwa na mjadala wa pamoja unaohusu wanawake na uongozi.

Alisema utafiti uliofanywa na Taasisi ya Uongozi unaonesha kuwa wanawake wapo wengi katika nafasi za chini za utendaji wanapoelekea nafasi za juu za uamuzi wanapungua.

"Tukasema labda tuongeze jitihada za kuwaweka zaidi katika programu ili waendelee kushika nafasi za juu. Katika kongamano hili la nne tumewaleta wabobezi watakaochangia mada yetu ya wanawake na mabadiliko," alisema Singo.

# Wenye ulemavu waonywa ulaghai kukubali mila, utamaduni potofu

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza mashirika mbalimbali vikiwamo vyama vya watu wenye ulemavu, kuachana na watu wasio na nia njema wanaotoa fedha nyingi katika taasisi hizo ili kuharibu mila na desturi za Watanzania.

Majaliwa aliyasema hayo jana, wakati akifunga Maadhimisho ya Wiki ya Fimbo Nyeupe ambayo kitaifa yaliadhimishwa mkoani Kilimanjaro.

"Tusikubali kabisa watu hao wanakuja kuharibu utamaduni wetu hasa katika mporomoko wa maadili. Tuwakatae. Huko nyuma tuliyumba kidogo, sitaki kutaja ni mambo gani, yote ninajua. Tupinge kwa nguvu matukio haya ili kulinda utamaduni," aliagiza.

Majaliwa alisema serikali katika mwaka huu wa fedha imetenga Sh. bilioni 20.21 kutoka Sh. bilioni 16.4 kwa mwaka wa fedha 2023/24, kwa ajili ya kuwakopesha watu wenye ulemavu ikiwa ni asilimia mbili ya mapato ya ndani ya kila halmashauri. Alikumbusha kwamba kuwa mikopo hiyo ilikuwa imesimamishwa ili kuweka mazingira rafiki ya kuwafikia walengwa.

Waziri Mkuu aliwataka wenye ulemavu kujitokeza kuchukua mikopo hiyo na kuzitaka halmashauri nchini kulipa kipaumbele kundi hilo. Alisema katika mwaka huu wa fedha, serikali imejipanga kujenga miundombinu fikivu ya elimu kwa kujenga vyumba vya madarasa 6,357, matundu ya vyoo 1,482, kumalizia mabwalo 362, kukamilisha mabweni 36 katika shule za sekondari.

Majaliwa alisema serikali imepanga kujenga shule mpya fikivu 184 na mabweni 186 ya shule za sekondari, lengo ni kuwawezesha watoto wenye ulemavu kupata elimu.

Aliziagiza taasisi za serikali zihakikishe zinapojenga majengo ya umma mfano shule, hospitali au ofisi kuzingatia maelekezo ya serikali ya kujenga miundombinu fikivu itakayowawezesha walemavu kufika.

Katika hatua nyingine, Majaliwa alisema serikali imejipanga kununua vifaa fikivu vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika shule za msingi 400 na sekondari 500 kuhakikisha watoto wasioona na wenye ulemavu wanapata haki ya elimu bora kama wengine.

Kaulimbiu ya mwaka huu ya maadhimisho hayo ilikuwa "Upatikanaji wa Teknolojia Saidizi na Fikivu ni Mkombozi kwa Uchumi Endelevu kwa Mtanzania Asiyeona'. Mkuu wa Mkoa huo, Nurdin Babu, akitoa salamu za mkoa, alisema kupitia mikopo inayotolewa mkoani humo, tayari watu wenye ulemavu wamepewa zaidi ya Sh. bilioni moja.

"Sisi tunaishi vyema na watu wenye ulemavu wakiwamo wasioona, tunaimarisha ulinzi wa maisha yao na kupinga ukatili, pia tunawaboreshea uchumi kwa kuhakikisha wanapata mikopo na kuingia kwenye TASAF (Mfuko wa Maendeleo ya Jamii)," alisema Babu.

Naibu Katibu wa chama hicho, Luata Lomitu, katika risala yao, alisema wanachama hao wanakabiliwa na matatizo mbalimbali yakiwamo yanayohusu miundombinu, kutopewa fursa za ajira, kukosekana kwa elimu kutokana kukosekana kwa vitendea kazi.

"Tunaiomba serikali kuandaa mwongozo na vifaa stahiki kwa wasioona, ili kuwajumuisha kwenye masuala ya kijamii, kisiasa ili kujikwamua na umaskini. Elimu iendelee kutolewa kwa jamii ili waweze kumtambua na kumsaidia mtu asiyeona hasa awapo barabarani," alisema.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Uyui, Said Ntahondi (katikati), akifafanua jambo kwa madiwani wenzake 60, walipofanya ziara ya kikazi kwenye Kampuni ya Alliance One Morogoro, juzi. Wa pili kulia ni Msemaji wa kampuni hiyo, Wakili John Magoti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Manispaa Moro kujenga stendi ya kisasa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro inakusudia kuanza ujenzi wa stendi mpya ya kisasa ili kuwapunguzia mzigo wa gharama wasafiri wanatumia usafiri wa treni ya kisasa (SGR).

Takriban wasafiri 10,000 wanaanzia safari zao mkoani Morogoro ili kwenda katika mikoa mingine.

Meya wa Manispaa ya Morogoro, Pascal Kihanga, alisema juzi kuwa ujenzi huo utaanza wakati wote kuanzia sasa baada kupatikana kwa mkandarasi na kuwataka wakazi wa manispaa hiyo kutumia fursa ya uwapo kwa SGR kubuni biashara mbalimbali zitakazowaingizia kipato.

Meya Kihanga alisema hayo wakati akizindua Duka la Kisasa la Kampuni ya Mawasiliano ya Simu ya Airtel Tanzania lililojengwa kwenye stendi ya SGR kwa ajili ya kurahisisha wasafiri wanaingia na kutoka nje ya mkoa wa Morogoro.

Alisema fursa nyingine ni pamoja na manispaa hiyo kuanza kujipanga kuwa Jiji tarajiwa kwa kuanza kuboresha miundombinu ya mawasiliano yatakayorahisisha wananchi kupata huduma za kijamiii.

"Niwaombe wananchi kuchangamkia fursa ya SGR inayofanya safari zake Morogoro, Dar es Salaam na Dodoma. Kwa siku kuna zaidi ya abiria 10,000 wanaingia na kutoka ambao wanakuja kuanzia safari zao kwenda mikoa mbalimbali.

"Wananchi wa Morogoro watumie nafasi hiyo kujipanga kufanya shughuli za ujasiriamali. Wasisubiri waje kutoka nje ya mkoa wakati wao wapo hapa hapa," alisema.

Meya Kihanga alisema manispaa imeboresha miundombinu ya mawasiliano ambayo kati ya kata 29, mpaka sasa ni kata moja tu yenye changamoto hiyo ambayo siku chache zijazo tatizo hilo litamalizika.

Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja wa Airtel Tanzania, Adriana Lyamba, alisema wameamua kuwasogezea huduma wasafiri wanaotumia treni hiyo ya mwendokasi kwenye stendi hiyo ili kupata huduma zote wakiwa kwenye maeneo bila kwenda mjini.

Alisema Airtel imekuwa ikiunga mkono jitihada mbalimbali za serikali ikiwamo kusogeza huduma kwa wananchi ili kuwapunguzia adha ya kutumia umbali mrefu kuzifuata huduma hizo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mungu ibariki Taifa Stars kuelekea fainali za CHAN

**WAKATI** vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga tayari wametinga hatua ya makundi katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Timu ya Taifa (Taifa Stars), inatarajia kushuka dimbani kesho ugenini kucheza dhidi ya wapinzani wao, Sudan.

Simba imetinga hatua ya makundi katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika wakati mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wao wametinga hatua hiyo kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Taifa Stars na Sudan zinakutana katika mechi ya kwanza ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), fainali hizo zitachezwa Februari, mwakani hapa Tanzania. Mechi hiyo ya kwanza itachezwa nchini Mauritania kwa sababu wenyeji Sudan wanakabiliwa na changamoto ya hali ya usalama nyumbani kwao na mchezo wa marudiano utafanyika Novemba 3, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Tayari Kocha Mkuu wa timu itakachoshiriki mashindano hayo, Bakari Shime, ameshatangaza kikosi chake kitakachosafiri kwenda kupeperusha bendera ya Tanzania katika michuano hiyo kinachoongozwa na aliyekuwa kipa chaguo la kwanza wa Simba, Aishi Manula.

Shime ameita wachezaji wachache wanaocheza katika timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, tena kutoka kwenye vilabu vidogo, na akijaza nyota wengi kutoka Ngorongoro Heroes, kikosi kilichotwaa ubingwa wa mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-20), ambayo yalimalizika hivi karibuni ili kutovuruga ratiba ya ligi hiyo.

Kocha huyo amesema kutokana na uhalisia, timu hiyo ilifanya mazoezi kwa muda mfupi hapa nyumbani kabla ya kusafiri kuwafuata Sudan, na alitarajia kwenda kukamilisha programu ya mazoezi Mauritania, lakini anaamini wachezaji wote wako tayari kuipeperusha bendera ya Tanzania kutokana na kuwa bado wana 'moto' wa kushindana.

Imezoeleka siku zote Stars inaundwa na nyota Wazalendo wanaofanya vizuri katika Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini safari hii imekuwa tofauti kwa sababu wachezaji waliotarajiwa kuitwa wanaonekana wanakabiliwa na uchovu unaotokana na kucheza mechi ngumu za mashindano mbalimbali hivi karibuni.

Shime ameweka wazi, milango kwa wachezaji wengine wanaocheza hapa nchini haijafungwa, akimaanisha atakifanyia maboresha kwa kukiongezea nguvu baada ya kumaliza mchezo wa kwanza bila ya kujali matokeo gani watayapata kesho.

Kiufundi huenda ameamua kuwaamini wachezaji vijana kwa sababu wanahitaji kujenga timu ya muda mrefu, lakini anawapa mapumziko nyota watakaocheza mechi ya marudiano kwa sababu watakuwa wamebaki hapa nyumbani, hawatakuwa na uchovu wa safari na fatiki ya mchezo wa kwanza ambao pia wanahitaji kupata matokeo chanya.

Kikubwa benchi la ufundi ambalo limepewa dhamana ya kukiongoza kikosi hicho ni kufanya kazi kwa kujiamini na kuwapa hamasa wachezaji kuwa wanaweza, waende Mauritania kwa kazi moja ya kulipigania taifa lao. Tunawakumbusha wachezaji wa Stars wafahamu hata mbuyu ulianza kama mchicha, mastaa ambao leo hii tunawaomba katika klabu na timu mbalimbali za taifa, walianza kama wao, wakionekana ni wachezaji chipukizi, lakini nafasi kama hii ambayo wamepata ndio wanatakiwa waitumie vizuri ili kujiweka sokoni.

Mchezaji yoyote anayevaa jezi ya taifa afahamu anakwenda vitani na anatakiwa kupambana bila kukata tamaa kwa kusaka matokeo chanya, wafahamu nafasi waliyopata si tu ya kulitangaza vyema jina la Tanzania kimataifa, lakini wanaenda kujiweka kwenye rekodi za kuipambania nchi.


Bila shaka tunaamini kikosi hicho kitakaporejea nchini, mashabiki wajitokeze kwa wingi kuwashangilia katika mechi ya marudiano, kwa kufanya hivyo kutawaongezea hamasa ya kufanya vyema na hatimaye kujiweka kwenye nafasi nzuri katika kampeni ya kuelekea fainali za CHAN.

Mungu ibariki Taifa Stars, Mungu Ibariki Tanzania katika safari ya kuelekea Fainali za CHAN 2025.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Kanuni ya kuita wachezaji Taifa Stars iangaliwe upya

**WACHEZAJI** wawili tegemeo wa Fountain Gate, Selemani Mwalimu na Edgar William wameitwa katika kikosi cha timu ya soka ya Taifa (Taifa Stars), kwa ajili ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Italazimika kucheza michezo mitatu bila ya washambuliaji hao nyota ambao kesho watapeperusha bendera ya Tanzania ugenini dhidi ya Sudan na katika mechi ya marudiano itakayochezwa baada ya wiki moja hapa nyumbani, kwa kiasi kikubwa ndiyo waliofikisha hapo ilipo.

Jana Fountain Gate ilicheza mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Singida Black Stars na keshokutwa watacheza mechi nyingine dhidi ya Mashujaa FC na Novemba 2, mwaka huu watavaana na Pamba Jiji ya Mwanza.

Selemani na Edgar watakuwa wameshakosa michezo hiyo mitatu kitu ambacho haikupaswa kitaipunguzia nguvu klabu yao.

Kwa matokeo yoyote ambayo Fountain Gate itayapata, haikupaswa kucheza bila wachezaji hao ambao ndiyo mhimili wa timu yenyewe.

Ikitokea ikapoteza michezo yake basi moja kwa moja sababu kubwa itakuwa ni kuwakosa wachezaji hao wa kikosi cha kwanza.

Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Bakari Shime, alisema hawakuita wachezaji wengi wanaocheza Ligi Kuu Bara ili kutoharibu ratiba.

Ukweli kanuni ya Ligi Kuu Bara inaruhusu timu kuendelea kucheza kama ina wachezaji wasiopungua watano, hivyo kwa sasa hakuna kilichokiukwa, lakini ukweli timu hiyo inaweza kujikuta inaumua kwa aina ya matokeo.

Fountain Gate ni timu ambayo haikudhaniwa kama ingeleta upinzani kwenye Ligi Kuu, lakini kwa namna ilivyoshangaza wengi imeonekana ni tishio, ikiwa na wachezaji mahiri wasiotegemewa.

Mwalimu ndiye kinara wa mabao kwa sasa wa Ligi Kuu, akipachika magoli sita, huku Edgar akifunga mabao manne, hivyo hao wawili tu wamechangia jumla ya mabao 10, kati ya 17 ambayo timu hiyo imeyafunga mpaka sasa.

Takwimu zinaonyesha Fountain Gate ndiyo timu iliyofunga mabao mengi zaidi katika Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa, ikifuatiwa na Simba yenye mabao 13 kabla ya mchezo wa jana dhidi ya Namungo.

Fountain Gate, kabla ya michezo ya jana ilikuwa inashika nafasi ya nne katika msimamo wa ligi hiyo, imecheza michezo nane na kujikusanyia pointi 16.

Imeungana na Singida Black Stars na Azam FC, kuwa timu ngumu na hatari zaidi msimu huu.

Niseme tu kanuni hii inapaswa kuangaliwa upya kuelekea msimu ujao. Nasema hivyo kwa hiki kilichojitokeza kwa sababu timu ikichukuliwa japo mchezaji mmoja tu inaweza kuiathiri moja kwa moja.

Simba na Yanga huwa hazipitii machungu ya kanuni hii kwa sababu wachazaji wao wengi huchukuliwa Stars na kupata nafasi ya michezo yao kuahirishwa, au wakati mwingine huwa ipo kwenye kalenda ya FIFA.

Timu za kati na za chini ndiyo zinaathirika zaidi na kanuni hii kama tunavyoona kwa wachezaji hao.

Ni wakati sasa kanuni itamke kuahirisha michezo kwa timu yoyote ambayo ina mchezaji kwenye kikosi cha timu ya taifa, kama michezo hiyo haipo kwenye kalenda ya FIFA kama tunavyoona kwenye mechi hizi.

Nimalizie kwa kusema timu zote 16 kwenye ligi zipo sawa na zina haki sawa, hakuna ambayo ina umuhimu zaidi ya kushinda kuliko mwingine, hakuna inayohitaji zaidi ubingwa na nyingine inasindikiza.

Kuwachukua wachezaji hao na ligi kuendelea ni sawa na kumpokonya silaha mwindaji kwenye msitu wenye wanyama wakali.

Kanuni siku zote si msahafu na mara nyingi hubadilika kutokana na makosa, changamoto na matukio yanayojitokeza ili kuendelea kuiboresha ligi yenye usawa na timu zote.

# HABARI KITAIFA

## Balozi afurahishwa na uhusiano wa Tanzania na Namibia kuimarika

**Na Maulid Mmbaga**

KAIMU Balozi wa Tanzania nchini Namibia, Elias Tamba, amesema amefurahishwa na namna Tanzania inavyoendelea kuimarisha misingi ya uhusiano wa diplomasia baina yake na nchi hiyo katika nyanja mbalimbali, huku mchango wa kusaidia uhuru wa Namibia ukitajwa.

Aliyasema hayo wakati Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga, alipotembelea Ofisi za Ubalozi wa Tanzania Nchini Namibia jana.

Alisema Tanzania itaendelea kushirikiana na Namibia katika masuala mbalimbali kwa kuzingatia urafiki ulioko baina ya mataifa hayo mawili toka kipindi ya uhuru ambako Tanzania inakumbukwa kwa mchango wake.

"Ninaishukuru serikali ya Tanzania kwa namna inavyoimarisha uhusiano wa kidiplomasia baina yake na Namibia, hii itasaidia kuchangamkia fursa za kimaendeleo zilizoko katika taifa hili ikiwamo masuala ya kibiashara," alisema Tamba.

Ummy alisema hatua hiyo imefikiwa kutokana na uongozi makini wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyojipambanua kidiplomasia.

Alisema Rais Samia amehakikisha uhusiano wa Tanzania na nchi nyingine ni wenye manufaa na kuiletea nchi heshima katika nyanja mbalimbali.

"Hakika Tanzania imeendelea kuwa kitovu cha amani na utulivu, hii imetokana na uongozi mahiri wa Rais Samia kwa miongozo na maelekezo yake katika kuhakikisha nchi inaendelea kujipatia maendeleo," alisema Ummy.

## Tanzania yaainisha vipaumbele vitatu CHOGM

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mahmoud Kombo, amesema miongoni mwa vipaumbele ambavyo Tanzania imeviainisha katika Mkutano wa Wakuu wa Serikali na Jumuiya ya Madola (CHOGM) ni pamoja na kuwezesha vijana na wanawake kiuchumi.

Vingine amevitaja ni kudhibiti mabadiliko ya tabianchi na kukuza matumizi ya teknolojia na kuimarisha ushirikiano wa biashara na uwekezaji kwa nchi wanachama.

Vipaumbele hivyo aliviwasilisha juzi katika mkutano wa mawaziri wa mambo ya nje na wanachama wa jumuiya ya madola, ajenda kuu ikiwa ni ustahimilivu katika kufikia malengo ya pamoja ya kimaendeleo 'One Resilient Common Future' pamoja na agenda nyingine zitakazojadiliwa katika vikao vya Wakuu wa Nchi.

Mkutano huo uliridhia agenda za; ustahimilivu wa mazingira, ustahimilivu wa uchumi, ustahimilivu wa watu katika jamii na ustahimilivu wa taasisi zinazolinda demokrasia, utawala wa sheria na haki za binadamu kuwekwa mezani kwenye mkutano wa ngazi za juu.

Katika mkutano huo, Waziri Kombo pamoja na Naibu Waziri Mkuu ambaye ni Waziri wa Mambo ya Nje wa Pakistan, Muhammad Ishaq Dar, walikubaliana kuongeza ushirikiano katika kilimo, teknolojia, viwanda vya nguo na biashara.

Waziri Kombo alishiriki pia, Mkutano wa Jukwaa la Biashara la Jumuiya ya Madola (CBF) uliowa kutanisha viongozi wa ngazi za juu wa Jumuiya ya Madola na kuzitaka nchi wanachama kuwa mstari wa mbele katika matumizi ya nishati safi ya kupikia kama moja ya mbinu za kufikia mpango wa jumuiya wa kuzalisha nishati endelevu.

Kadhalika aligusia changamoto kubwa ni ukubwa wa gharama za nishati safi ya kupikia, suala la tamaduni na mazoea ya watu kutumia kuni au mkaa kupikia na hivyo kuchelewesha Tanzania kufikia mabadiliko yanayokusudiwa kwa haraka.

Kombo alialika Jumuiya ya Madola kutumia fursa za ushirikiano katika nishati pamoja na uwekezaji nchini Tanzania.

Mkutano huo ulihudhuriwa na Lord Collins of Highbury ambaye alisema Uingereza imejipanga kuongeza idadi ya watu wenye ujuzi zaidi wa masuala ya nishati ili kudhibiti mabadiliko ya tabianchi.

Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola, Dk. Arjoon Suddhoo, aliunga mkono mjadala huo, akisisitiza kusaidia Jumuiya ya Madola kuona ni kwa namna gani inaweza kushirikiana kukuza matumizi ya nishati endelevu kufikia mwaka 2030.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Zanzibar, Shaaban Ali Othman, alishiriki Mkutano wa Mawaziri wa Nchi Ndogo za Jumuiya ya Madola.




Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, akizungumza wakati akifunga mafunzo ya wanawake wajasiriamali wa Ilala, yaliyotolewa bure na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## RC Chalamila ataka ujenzi wa barabara mwendokasi kufanyika usiku na mchana

**Na Joseph Mwendapole**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amemwagiza mkandarasi anayejenga barabara ya mabasi ya mwendokasi (BRT -3) kufanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha kazi mapema mwakani kwa mujibu wa mkataba.

Mradi huo unaoanzia Posta katikati ya jiji la Dar es Salaam kwa kilomita 23 kupitia Tazara hadi Gongo la Mboto, unajengwa na kampuni ya China ya M/S Sinohydro Cooperation Limited.

Chalamila alitoa agizo hilo juzi wakati wa ziara yake kwenye miradi mbalimbali jijini Dar es Salaam katika Wilaya ya Ilala ambayo amekuwa akiifanya nyakati za usiku.

Alisema kipindi cha mvua kinatarajia kuanza hivi karibuni, hivyo lazima mkandarasi ajipange kuhakikisha anafanya kazi kwa kasi na kuweka mazingira ambayo yatamfanya aendelee kufanya kazi hata wakati wa mvua hizo.

"Nimekuja hapa nimewakuta mnafanyakazi usiku. Sasa naomba mwendelee hivi hivi usiku na mchana. Sitaki visingizio vyovyote, nataka barabara hii ikamilike kwa wakati ili wananchi waanze kunufaika nayo na kuondokana na adha ya foleni," alisema.

Pia aliwapongeza wahandisi wa Wakala wa Barabara (TANROADS) ambao wamekuwa wakiwasimamia makandarasi usiku na mchana ili mradi ukamilike kwa wakati na kwa viwango vilivyowekwa kwenye mkataba wa ujenzi huo.

"Nitaendelea kutembelea miradi hii kwa mtindo wa kushtukiza ili nione kama mnafanya kazi usiku kwa sababu mmesikia ninakuja leo au ni kawaida yenu na TANROADS hakikisheni ujenzi unazingatia viwango kwa sababu fedha zinazowekwa hapa ni mabilioni," alisema.

Meneja Mradi wa BRT-3 kutoka TANROADS, Frank Mbilinyi, alimhakikishia Chalamila kuwa mradi huo unatarajiwa kukamilika kwa wakati na kuanza kazi kuanzia mwishoni mwa Februari, mwakani na kwamba sehemu kubwa ya barabara inayojengwa itakamilika Desemba, mwaka huu.

"Nikuhakikishie Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, mkandarasi anakwenda kwa kasi nzuri na sisi wasimamizi kwa upande wetu tumekuwa tukishirikiana naye kuhakikisha fedha zinatoka kwa wakati na mradi hausimami na tunaamini utakamilika kwa wakati," alisema Mbilinyi.

Chalamila pia alitembelea barabara ya BRT-4 inayoanzia Mwenge hadi Tegeta DAWASA inayojengwa na kampuni ya M/S Shandong Luquiao Group Co Ltd yenye urefu wa kilometa 15.63.

Alimtaka mkandarasi huyo kuweka rasilimali watu ya kutosha ili kuhakikisha kazi inafanyika haraka kabla ya kuanza kwa msimu wa mvua ili kuepuka kuchelewesha kukamilika kama ilivyopangwa kwenye mkataba.

"Hakikisheni mnazingatia kila kilichokubaliwa kwenye mkataba wa ujenzi na kama rasilimali watu ni ndogo, ongezeni na mfanye kazi usiku na mchana," alisisitiza.

# Pinda ataka NHC kujenga nyumba kwenye miji kulingana na mahitaji

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, amelitaka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kujenga nyumba zenye uhitaji katika maeneo ya mijini.

Pinda alitoa agizo hilo juzi jijini hapa wakati akikabidhi hati miliki za ardhi kwa wananchi walionunua viwanja kupitia Mradi wa Safari City unaotekelezwa na NHC.

Jumla ya hati 240 zilishagawiwa kwa wanunuzi wa viwanja katika mradi huo na katika tukio hilo, Naibu Waziri alikabidhi hati milki 30 kati ya 81 zilizoandaliwa.

"Vijumba vingine vilivyoko katikati ya mji kwa kweli ni kama vile vya urithi. Havina sura ya Tanzania ya sasa. Mwende mkawaze upya ili tupate thamani inayofanana na uhalisia," alisema.

Pinda aliitaka NHC kutouza nyumba zilizoko katikati ya miji badala yake izibomoe na kujenga upya kulingana na uhitaji wa maeneo husika.

"Ukiweka hata ukumbi utapata wapangaji wengi. Ukijenga hoteli watu watakuja kupanga na kuendesha shughuli zao," alisema Pinda.

Meneja wa NHC Mkoa wa Arusha, Benit Masika, alisema shirika hadi sasa limeuza viwanja 1,026 na kati ya hivyo, 350 wateja wake wamemaliza malipo kwa asilimia 100.

"Naomba ieleweke kwamba NHC imeazimia kuuza viwanja kwenye mradi huu wa Safari City kwa malengo ya kutoa fursa ya uendelezaji kwa wananchi wa wadau," alisema Masika.

Kwa mujibu wa Masika, NHC katika mkoa wa Arusha, mradi wa Safari City tayari umefikiwa na huduma wezeshi kwa wateja kama vile maji, umeme na miundombinu ya barabara ambayo alisema imekuwa ikiendelezwa na serikali ili kuwawezesha walionunua maeneo kuendeleza maeneo yao.

" Shirika limetenga viwanja 1,601 kwa ajili ya kuviuza na viwanja 313 shirika limehifadhi kwa ajili ya uendelezaji wa baadaye," alisema.

Baadhi ya wanunuzi wa viwanja kupitia mradi huo wa Safari City wamefurahi na kuishukuru serikali kwa kuwakabidhiwa hati milki za ardhi katika eneo hilo walilolielezea kuwa limepangiliwa vizuri na NHC.

Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Mkoa wa Arusha, Lorivii Long'idu, ambaye taasisi yake ni moja waliokabidhiwa hati kupitia mradi wa Safari City, alisema ofisi yake baada ya kukabidhiwa hati milki, itaanza ujenzi wa ofisi ya kanda ikiwa ni kuunga mkono juhudi za serikali ya mkoa.

"Jengo hili litakapokamilika litakuwa likitoa huduma (za EWURA) katika Kanda ya Kaskazini," alisema Long'idu.

Mradi wa Safari City ulioandaliwa eneo la ekari 587 katika mpango kabambe ulioandaliwa mwaka 2014 uko eneo la Burka Mateves ndani ya Jiji la Arusha.

Mradi huo una viwanja 1,913 kwa ajili ya uendelezaji wa nyumba za makazi, majengo ya biashara, huduma za jamii kama vile shule, vyuo, hospitali, sehemu za ibada, viwanja vya michezo, kupumzikia na maeneo ya usalama wa miji kama vituo vya polisi, zimamoto na viwanda vidogo vidogo.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda (kushoto), akikabidhi hati milki ya ardhi kwa Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Mkoa wa Arusha, Lorivii Jeremiah Long'idu, wakati wa hafla ya kukabidhi hati kwa wananchi walionunua viwanja kupitia mradi wa Safari City Arusha, juzi. **PICHA: WANMM**

# Mpogolo afunda wajasiriamali wanawake

**Na Joseph Mwendapole**

MKUU wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, amewataka wajasiriamali kutumia elimu ya bure waliyopewa na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), kukuza biashara zao na kuyafikia masoko ya kimataifa badala ya kuendelea na mtindo wa kufanya biashara kwa mazoea.

Aliyasema hayo jana wakati akifunga mafunzo ya siku tatu kwa wanawake wajasiriamali zaidi ya 600 wa wilaya ya Ilala yaliyoendeshwa chuoni hapo bure kwa wajasiriamali wanawake.

Mpogolo alisema imekuwa kawaida kwa wajasiriamali wengi wanawake kufanya biashara kwa mazoea bila kuwa na ujuzi wowote lakini mafunzo hayo yamewafungua macho na kupata ujuzi wa namna ya kupata masoko.

"Wilaya ya Ilala na Jiji tumefurahishwa na mpango huu wa CBE na Mkurugenzi na timu yake wamefurahishwa sana pia na wanawaunga mkono kwenye mpango huu wa kuwasaidia wajasiriamali," alisema.

Pia alisema amezungumza na Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Edda Lwoga, kuangalia namna ya kupeleka elimu hiyo kwenye kata za pembezoni ili wanawake wengi wanufaike na elimu hiyo.

"Nimefurahi sana kuona wamepewa elimu ya mikopo kwa sababu kwetu Ilala tumetenga Sh. bilioni 11 kwa ajili ya kukopesha wajasiriamali kwa hiyo elimu hiyo waliyopata inatupa uhakika kwamba watafanyabiashara na kurejesha mikopo yao," alisema.

Mpogolo pia alisema kwenye mikopo itakayotolewa, serikali imewatenga wajasiriamali hao kwenye makundi matatu kundi la kwanza likiwa lile la wajasiriamali watakaopata mkopo wa kuanzia Sh. 500,000 hadi milioni 10.

Alitaja kundi lingine kuwa ni la wajasiriamali watakaopata mkopo wa kuanzia Sh. milioni 10 hadi milioni 50 wakati kundi la tatu ni la wajasiriamali watakaokopa kuanzia Sh. milioni 50,000,000 hadi 150.

"Sisi tumeona tusisitize kundi la kwanza lenye wanawake wengi ambao wamekuwa wakichukua mikopo umiza ambao wengi wao wanachukua kuanzia Sh. 20,000, wengine 50,000 na wengine 100,000 au 200,000 wanachukua fedha kidogo sana lakini ni kundi kubwa sana," alisema.

Naye Prof. Lwoga alisema wamekuwa wakitoa mafunzo ya ujasiriamali kwa makundi mbalimbali ya wanawake, vijana kwa ajili ya kuwajengea uwezo ili kuimarisha biashara zao.

"Tunafahamu kwamba kwa kuwajengea uwezo tutakuwa tumewezesha kuchochea uchumi wa mtu mmoja mmoja na wa familia na kwa taifa kwa ujumla, leo tumeanza na Ilala kuwajengea uwezo wajasiriamali 600. Tumewafundisha namna ya kufungasha biashara, kutafuta masoko, kutunza fedha na kurejesha mikopo kwa wakati," alisema.

Pia alisema wamewafundisha pia namna ya kutengeneza mpango bora wa biashara na aliishukuru Wilaya ya Ilala ambayo imeshirikiana kwa karibu na Chuo cha CBE kuwapata wajasiriamali hao ambao wamepata mafunzo ya siku tatu.

Alisema mafunzo hayo yatakuwa endelevu kwenye kampasi za CBE katika mikoa ya Dodoma, Mwanza na Mbeya ambayo wajasiriamali 600 wa mikoa hiyo nao watanufaika na mafunzo ya aina hiyo.

Meneja Mafunzo wa Benki ya Equity, Martin Rajabu, alisema benki hiyo inaona fahari kuungana na CBE kutoa elimu ya ujasiriamali nchi nzima kwa kuwa wanawake wengi wanafanyabiashara bila kuwa na ujuzi unaohitajika.

# Walia kushuka kwa bei dengu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
ITIGI

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi mkoani Singida, wameilia Wizara ya Kilimo na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Tanzania (CPB) kutaka iingilie kati kunusuru mdororo wa bei ya dengu ambayo imeshuka ghafla na kusababisha wakulima kushindwa kupata soko kuuza.

Wakizungumza jana katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo, walisema suala hilo la dengu limewaweka katika wakati mgumu kisiasa kutokana na kushuka bei. Bei ya zao hilo katika soko la mwisho iliuzwa Sh. 1,620 kwa kilo.

"Madiwani tuko katika hali ngumu kisiasa kwa sababu dengu imeporomoka bei. Mkulima akitaka kuuza hata gunia moja au mawili kupata fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida, hakuna pa kuuza," alisema Ally Minja, ni Diwani wa Itigi Mjini.

Alisema ili kunusuru hali hii katika kipindi hiki cha kuelekea mwisho mwa msimu, serikali ingeruhusu wanunuzi binafsi ili wakulima ambao bado wameweka dengu majumbani, wanunue kwa kuwa hivi sasa wafanyabiashara waliokuwa wakinunua wamehamia kununua korosho.

"Tuwasiliane na mamlaka akiwamo mkuu wa mkoa kuona namna gani tutawasaidia wakulima wa dengu maana kinachoendelea hata halmashauri hatupati mapato," alisema.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, Jonathan Dulle, alisema Wizara ya Kilimo na CPB zina uwezo wa kusaidia wakulima katika changamoto hiyo ya kuporomoka kwa bei.

"Hatuwezi kukusanya mapato nje ya mfumo wa stakabadhi ghalani. Tutaendelea kutumia mfumo huu na kimsingi watendaji wetu wamefanya vizuri sana na ziko AMCOS (vyama vya ushirika vya msingi vya mazao) zimefunguliwa kwenye maeneo mengi ambako kila mkulima anaweza kupeleka mazao yake kwenda kuuza," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Dk. Vicent Mashinji, alisema changamoto zilizojitokeza msimu huu wakati wa kuuza dengu kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani mwakani kutakuwa na maboresho ambayo hayataleta changamoto tena.

Mkoa wa Singida ulizindua rasmi utekelezaji wa mfumo wa stakabadhi ghalani kwa msimu 2024/25 kutokana na maagizo yaliyotolewa na serikali kupitia mwongozo wa biashara ya dengu, mbaazi na ufuta.

Mwongozo huo ulitolewa chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) na Soko la Bidhaa (TMX).





# Kamati yapokea mapendekezo mpango wa maendeleo ya taifa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Bajeti imepokea mapendekezo ya serikali kuhusu mpango wa maendeleo wa taifa wa mwaka 2025/26 unaolenga masuala mbalimbali ikiwamo kuimarisha uwekezaji nchini.

Kwa mujibu wa kanuni ya 113(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Februari 2023, mapendekezo ya mpango huo yanawasilishwa kwa kamati hiyo ili kupata maoni ya wabunge katika maandalizi yake.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, akizungumza katika kikao cha kamati alichoambatana na Katibu Mkuu, Dk. Tausi Kida, Menejimenti ya Ofisi hiyo na Tume ya Mipango, alisema katika kuhakikisha ufanisi wakati wa utekelezaji wa mpango huo, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi itaweka mkazo katika maeneo ya miradi ya kielelezo yenye manufaa na matokeo makubwa.

Alisema mapendekezo hayo yanatoa msingi wa maandalizi wa mpango wa maendeleo wa taifa wa 2025/26 kuimarisha uwekezaji katika nyanja mbalimbali ili kuwa na uchumi imara na stahimilivu, kuimarisha uzalishaji viwanda na huduma bora kwa Watanzania. "Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 yanaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inayolenga kuwezesha Tanzania kuingia katika kundi la nchi za uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 na kuwa na kiwango cha juu cha maendeleo ya watu."

"Mapendekezo ya mpango yamejikita katika kuendeleza na kukamilisha utekelezaji wa afua zinazotoa matokeo ya maeneo matano ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano," alisema.

Prof. Mkumbo alisema mafanikio ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa mwaka 2023/24 kwamba serikali ilipanga kutekeleza miradi 17 ya kielelezo inayolenga kuleta matokeo katika maeneo hayo matano ya kipaumbele ikiwa ni miradi ya miundombinu ya usafiri na usafirishaji na ile ya kuongeza uzalishaji viwandani.

Pia alisema mwenendo wa hali ya uchumi wa dunia na ule wa taifa inaonesha kuimarika kwa uchumi na kupungua kwa mfumuko wa bei.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Oran Njeza, aliipongeza ofisi hiyo kwa wasilisho la Mpango wa Maendeleo ikiwamo taarifa ya ziada kuhusu mwenendo wa miradi ya maendeleo ambayo serikali inashirikiana na sekta binafsi.

Katika hatua nyingine, wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti Florent Kyombo, walipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo na kujadili mchakato wa uandishi wa Dira ya Maendeleo 2050 baada ya kuelezwa hatua iliyofikiwa.

# Bilioni 8/- kutekeleza mradi wa jinsia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHILINGI bilioni nane zinatarajiwa kutumika kutekeleza mradi wa 'Tuinuke Pamoja' wenye lengo la kutatua kero za kijinsia katika ngazi ya jamii kwa kipindi cha miaka mitatu mkoani hapa.

Meneja mradi huo, Nestory Mhando, alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mradi huo unaofadhiliwa na Ubalozi wa Ireland.

Alisema utekelezaji unafanywa na mashirika mawili ambayo ni Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na Aga Khan Foundation (AKF) na utapeleka rasilimali fedha kwa vikundi ambavyo viko katika ngazi ya jamii vilivyojikita na kupambana na kero za usawa wa kijinsia.

"Tunalenga pia kuinua wanawake kuwapatia fedha kupitia vikundi, kuwajengea uwezo na taaluma stahiki kwenye utekelezaji wa hiyo miradi ambayo wao watakuwa wamebuni.

**"Tunalenga pia kuinua wanawake kuwapatia fedha kupitia vikundi, kuwajengea uwezo na taaluma stahiki kwenye utekelezaji wa hiyo miradi ambayo wao watakuwa wamebuni.**

"Lakini eneo lingine ni kuviunganisha hivi vikundi pamoja na mitandao inayohusiana na masuala ya jinsia na haki za wanawake watoto lakini pia watu wote kwenye jamii ili mashirika hayo makubwa yajifunze lakini pia vile vikundi vijifunze kutoka kwa mashirika hayo makubwa hatimaye uzoefu wa pamoja utusaidie kuondoa changamoto za kijinsia katika jamii yetu," alisema Mhando.

Pia alisema kutakuwa na majukwaa ya mijadala ambayo yataleta pamoja serikali, wadau wa maendeleo, wanaharakati, vikundi na wanajamii ili kuangalia masuala ya kijinsia.

"Kwa huu mwaka wa kwanza, kiasi ambacho tunaenda kukitumia ni takribani Sh. bilioni mbili ambazo asilimia 50 zitakwenda moja kwa moja kwenye ile jamii tunayoilenga kwa maana ya kwamba hivi vikundi ambavyo vimejikita kwenye masuala ya kijinsia kwa sababu ndicho tunachokitaka na tunataka rasilimali nyingi iende huko," alisema.

Alisema katika mwaka wa pili na wa tatu, wanatarajia kuwa na kiasi kingine ambacho kitakamilisha jumla ya Sh. bilioni nane, ambazo zimewekezwa ili kuwa na jamii yenye usawa.

Ofisa Habari na Mratibu wa Mradi huo kutoka TGNP, Monica John, alisema mradi huo utatekelezwa kwa ushirikiano wa mashirika hayo ili kuwezesha vikundi katika ngazi ya jamii kuwa na harakati za pamoja za kuleta usawa wa kijinsia.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa (katikati), akizindua mradi wa maji katika kijiji cha Nkalakala, wilayani Mkalama, mkoani Singida jana. Mradi huo, wenye tangi lenye uwezo wa kuhifadhi lita 90,000 umegharimu Sh. milioni 348.9 na utahudumia vituo 12 vya kuchotea maji. Kushoto ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida, Martha Mlata. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Tanzania mwenyeji mkutano wa mtandao rasilimali watu Afrika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TANZANIA inatarajiwa kuwa mwenyeji wa mkutano wa tisa wa mtandao wa wasimamizi na mameneja rasilimali watu katika utumishi wa umma barani Afrika utakaofanyika kwa siku nne jijini Arusha.

Mkutano huo unalenga kubadilishana uzoefu na utaalamu ili nchi zipige hatua ya maendeleo kwa kutumia mbinu za kisasa za rasilimali watu.

Akizungumza jana jijini hapa, Rais wa Mtandao huo ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Xavier Daudi, alisema mkutano huo utafanyika Novemba 4 hadi 7, mwaka huu, na kuhudhuriwa na zaidi ya watu 400.

Alisema mkutano unalenga kuendeleza malengo muhimu ya kimkakati kwa maendeleo endelevu ya usimamizi wa rasilimali watu katika sekta ya umma barani Afrika.

"Mkutano huu utawakutanisha mawaziri katika sekta ya umma, makatibu wakuu, wanataaluma na wataalamu mbalimbali wa Afrika na kaulimbiu ni 'Uhimilivu wa Utawala na Ubunifu Kukuza Sekta ya Umma Yenye Uelekeo wa Baadaye Kupitia Uongozi wa Rasilimali Watu'. Niwaalike wataalamu wote kujisajili kuhudhuria mkutano huu muhimu wa kubadilishana uzoefu na utaalamu," alisema.

Awali, alisema historia ya mtandao huo imetokana na mkutano uliofanyika Eswatini mwaka 2017 wa Mawaziri wa Utumishi wa Umma ambao walikuja na wazo la kuwapo na mtandao ili kusaidia kuharakisha maendeleo barani humo.

"Mtandao huu uliundwa rasmi katika mkutano uliofanyika Arusha na tulipata bahati ulivyoanzishwa Rais wa kwanza alikuwa George Yembesi aliyekuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Mtandao ulianzishwa kwa lengo la kutafsiri mikakati ya kimaendeleo ya kitaifa, kikanda na kimataifa ili kujenga uwezo wa rasilimali watu yenye matokeo chanya kuhudumia watu barani Afrika," alisema.

Alisema mtandao huo una malengo mahsusi ya kubadilishana utaalamu, uzoefu na mbinu za kisasa katika uendeshaji wa rasilimali watu kwenye utumishi wa umma kupitia utafiti na mbinu mbalimbali zinazojitokeza duniani.



## UWT yapongeza kuanza kwa kilimo cha mpunga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UMOJA wa Wanawake Tanzania (UWT) umesema kitendo cha Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kuikaribisha Iran katika sekta ya kilimo cha mpunga cha umwagiliaji, kutaiondolea Zanzibar upungufu wa mchele na bei za bidhaa hiyo kushuka.

Mwenyekiti wa UWT Mkoa Kaskazini Unguja, Maryam Muharami Shomari, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari visiwani hapa. Alisema Dk. Mwinyi kukutana na wataalamu wa kilimo toka Iran ni ishara ya mafanikio makubwa.

Maryam alisema idadi kubwa ya wananchi wa Unguja na Pemba wanatumia mchele kama chakula kikuu, hivyo aina hiyo ya nafaka ina watumiaji wengi visiwani humo.

"Hatuwezi kuendelea kutegemea bidhaa kama mchele uagizwe toka nje wakati ardhi ipo yenye kuzalisha zao hilo. Uamuzi wa SMZ kukutana na wataalamu hao wa kilimo ni faraja kubwa kwa wananchi," alisema.

Mwenyekiti huyo pia alisema hata Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, aliwahi kusema Zanzibar inaweza hata kulima kilimo cha ngano na kumea lakini ndoto yake haikutimia kutokana na kifo chake mwaka 1972.

"Zanzibar tunaweza kulima kilimo chochote na kuzalisha idadi kubwa ya mazao ya kilimo. Wataalamu wetu wa ndani waishauri serikali aina ipi ya kilimo ili wakulima waanze kulima," alisema.

Alisema ikiwa Zanzibar itazalisha kwa wingi mahindi, mchele, sukari, matunda, manukato na karafuu, itasaidia kukuza uchumi na kupungua kwa bei za bidhaa hasa vyakula na kumpa unafuu mlaji.

"UWT tunaridhishwa na mikakati ya kisera ya serikali ya awamu ya nane. Tunamwomba Rais Dk. Mwinyi asisikilize maneno yanayokatisha tamaa. Aendelee na mkakati wa kazi zake kwani yajayo yatafurahisha zaidi," alisema.

Hata hivyo, alisema mradi kama huo ulianzishwa na serikali ya awamu ya pili ya Tanzania kwa kilimo cha mpunga cha umwagiliaji na wataalamu toka Iran Ikwiriri, Rufiji mkoani Pwani.

Alisema mradi huo wa kilimo ukianza Unguja na Pemba, utawanufaisha wakulima wengi na kuwapa manufaa makubwa kwa kuhifadhi chakula lakini kupata soko la bidhaa kwa wafanyabiashara na kuwaingizia kipato

# Klabu zasaidia hifadhi ya mazingira

**Na Rahma Suleiman, aliyekuwa** MUHEZA

KLABU za Mazingira (ECO SCHOOLS) katika shule za msingi wilayani Muheza zimesaidia kunusuru mng'onyoko wa udongo ambao ulikuwa ukiwaathiri wanafunzi na walimu shuleni.

Wanafunzi wa Shule ya Msingi Msasa IBC na Shule ya Msingi Kwezitu zilizoko Tarafa ya Amani wilayani humo, walisema kupitia klabu hizo wamepata elimu ya uhifadhi wa mazingira ambao umebadili mitazamo, tabia na mienendo yao na kwa sasa ni mabalozi wazuri wa utunzaji mazingira.

Waliyasema hayo wakati wakizungumza na waandishi wa habari wa chama cha waandishi wa habari za mazingira Tanzania waliofika wilayani humo kwa ziara maalum ya kimafunzo kuangalia maendeleo ya mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili.

Upendo Sangoda, mwanafunzi wa darasa la sita shuleni hapo, alisema awali mazingira ya shule hiyo yalikuwa hayaridhishi kutokana na mmong'onyoko wa udongo uliokuwa ukiwaathiri shuleni hapo.

Alisema mbali na mazingira ya shuleni, walikuwa wakienda msituni kuwinda ndege, kukata miti na uharibifu mwingine lakini elimu waliyoipata kupitia klabu za mazingira kumesaidia kuhifadhi mazingira na kunusuru mmong'onyoko wa udongo kwa kupanda nyasi.

"Nimejifunza kupanda miti kunatuletea mandhari nzuri na kutupatia kipato kwa sababu watalii wengi watakuja kutalii lakini pia msitu utatupatia wanyama na viumbe wengine," alisema.

Pia alisema ufugaji wa nyuki pia unasaidia katika uhifadhi wa mazingira na ukataji wa miti utasababisha majanga na viumbe hai pamoja na wanyama watatoweka.

Jackline Shetui, mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Kwezitu ambaye ni mjumbe wa kamati ya mazingira, alisema elimu aliyoipata imemsaidia kuwa balozi mzuri wa mazingira kuanzia shuleni hadi nyumbani.

Alisema atahakikisha anaitumia nafasi yake kuwaeleza wanafunzi wenzake umuhimu wa watoto kutunza mazingira ili kuepukana na majanga mbalimbali ikiwamo ukame.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi IBC Msasa, Barnaba Mloka, alisema kabla ya Mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili ambao umefanikisha kuundwa kwa klabu ya mazingira shuleni hapo, hali ilikuwa tete kutokana na mmong'onyoko wa udongo.

Mwalimu Mloka alisema mbali na kupata elimu ya kutunza mazingira, pia mradi huo umewasaidia kupata elimu ya kufuga nyuki na kuwezeshwa mazingira rafiki.

Akizungumzia mabadiliko yaliyopatikana kupitia klabu hizo, alisema watoto wameacha kuwinda ndege na sasa ni mabalozi wazuri wa kulinda na kuhifadhi mazingira.

Mwalimu wa Mazingira wa Shule ya Msingi Msasa IBC, Mariam Shekuamba, alisema licha ya klabu za mazingira kutoa elimu ya uhifadhi pia imesaidia kuwafundisha wanafunzi umuhimu wa utalii wa ndani.

Alisema katika kusoma kwa vitendo huwachukua wanafunzi mara moja kwa wiki kwenda milimani kuangalia ndege, miti na viumbe hai vingine vilivyoko ambapo imesaidia wanafunzi kuachana na tabia ya kwenda kuwinda ndege na badala yake wakiujua umuhimu wa ndege kwenye utalii.

"Sasa hivi hawawindi tena ndege, badala yake wamekuwa walinzi wa ndege hao na hii ni kwa sababu nimekuwa nikiwaambia kuwa viumbe hai jamii ya ndege ni muhimu kwa maisha ya binadamu. Zamani walikuwa wanaacha kuja shule wanakwenda kuwinda ndege, hali ni tofauti kwa sasa, badala ya kwenda kuwinda wamekuwa wakiomba kwenda kufanya utalii," alisema Shekuamba.




Padri Cosmas Alphonce Shayo (wa pili kushoto), akibadilishana mawazo na wajumbe wa kamati ya kitaifa ya Shirika la Mtakatifu Augustino, baada ya kuwasili kwenye Kanisa la Minara Miwili, mjini Zanzibar jana. Jumla ya wazee na wastaafu zaidi ya 400 wa shirika hilo, kutoka mikoa yote ya Tanzania walifanya ziara ya hija, kisiwani humo. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Mwinyi aagiza ulinzi wa miundombinu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameiagiza Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kusimamia hifadhi za barabara na kuzuia wananchi kujenga na kufanya biashara katika maeneo hayo.

Hatua hiyo amesema itapunguza mzigo mkubwa wa fidia kwa serikali pale inapotaka kupitisha miundombinu mingine muhimu.

Amesema hivi sasa kumezuka tabia ya wananchi kuzitumia hifadhi za barabara kwa kujenga na kufanya biashara bila kujali umuhimu wa hifadhi hizo na wakati mwingine kuziathiri barabara zilizojengwa.

Dk. Mwinyi alitoa agizo hilo alipofungua barabara mpya ya Jozani - Charawe- Ukongoroni hadi Bwejuu, mkoa wa Kusini Unguja yenye urefu wa kilometa 24.5.

Alisema wananchi wana wajibu mkubwa wa kutunza barabara zinazojengwa katika maeneo yao, kuonesha kuthamini juhudi kubwa zinazochukuliwa na serikali kuwajengea miundombinu bora ya usafiri na kuwaondoshea usumbufu waliokuwa wakiupata siku za nyuma.

Pia aliwahakikishia wananchi kwamba serikali itaendeleza ujenzi wa miundombinu ya barabara nchi nzima na kuwasisitiza kuunga mkono juhudi hizo.

Rais Dk. Mwinyi aliwathibitishia wananchi wa mkoa wa Kusini Unguja kuwamalizia barabara ya Tunguu - Makunduchi kwa kiwango cha njia nne zenye taa kutoka Mwanakwerekwe hadi Makunduchi.


Kuhusu tatizo la maji kwa mkoa huo, Dk. Mwinyi, alisema tayari serikali imejenga skimu nne kuu za maji safi ambazo zitamaliza tatizo la maji mkoani humo.

Alisema serikali inatambua tatizo la umeme mdogo katika mkoa huo kwa muda mrefu na kwamba imeshanunua "Grid Stabilization" na amefarijika kusikia tatizo hilo limeanza kupungua katika baadhi ya maeneo ya mkoa huo.

Pia Dk. Mwinyi ameridhia ombi la wananchi wa kusini la kujengewa daraja litalounganisha mkoa huko na wa Kaskazini Unguja ili kurahisisha mawasiliano baina ya hiyo na huduma zingine za uchumi na jamii.

Alibainisha kuwa tayari msanifu amekamilisha michoro na kuiwasilisha kwa serikali kwa hatua za awali na kuwahakikishia wananchi kuwa serikali inasubiri kujua gharama ili hatimaye kulijenga daraja hilo.

Akigusia sekta ya elimu, Rais Dk. Mwinyi aliwaahidi wananchi wa Zanzibar kuwa awamu ya pili ya ujenzi wa shule za ghorofa 26 iko mbioni na mkoa wa Kusini Unguja utakuwa miongoni mwao.



**GIGGY**
UKURASA 12

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE





# RUNGU LA MZEE PEMBE
# Liwekwe Makumbusho ya Taifa

WIKI hii tasnia ya uigizaji  na vichekesho imempoteza msanii mkongwe, Yusuph Kaimu, maarufu Mzee Pembe, ambaye amefariki dunia baada ya kuugua kwa muda mfupi.

Kifo chake kimeleta mshtuko katika fani ya uigizaji nchini, kutokana na ukweli kuwa Mzee Pembe alikuwa na kipaji kikubwa cha uchekeshaji, kitu ambacho ilikuwa vigumu kuchoka pale alipokuwa akiburudisha.

Akiwa na kawaida ya kushika rungu mkononi mwake na kugeuza silaha yake pale inapotokea sitofahamu, ni dhahiri wengi hawatamsahau na wanabaki kumshukuru kwa kile alichokifanya wakati wa uhai wake.

Hata hivyo, mustakabali wa rungu ambalo Mzee Pembe alikuwa akilibeba kila mara limeibua mjadala mkali, kufuatia familia ya msanii huyo kueleza wanaangalia namna ya kumkabidhi Rais Samia Suluhu Hassan, ili kuliweka kama makumbusho.


Pamoja na familia ya Pembe kuwa na nia njema ya kumuenzi baba yao, kuna baadhi ya watu wameonyesha wasiwasi kuwa uamuzi huo hautaweza kutekelezwa.

Hata hivyo, wengine wamesema kuwa uamuzi huo uko sahihi kutokana na Mzee Pembe kuwa miongoni mwa waigizaji wakongwe waliofanikiwa kufanya mambo makubwa kwa miongo kadhaa.

Wanasema wanafamilia hao wanatakiwa kuungwa mkono kwani hata kama Rais hatajitokeza na kuchukua, lakini, wizara husika inaweza kufanya hivyo na rungu hilo likawekwa makumbusho kwa manufaa ya vizazi vinavyokuja.

BASI SAWA

## Giggy Money hamtaki Cardi B



MWANAMUZIKI wa kizazi kipya Giggy Money, amesema hawezi kuacha kufuatilia vikoba vinavyompatia pesa kwa sababu ya rapa maarufu wa Marekani Cardi B.

Giggy amesema hayo baada ya mashabiki wengi wa muziki kumfananisha kwa mwonekano wake na msanii huyo maarufu duniani.

"Mimi sina muda wa kumfuatilia Cardi B kwa namna yoyote, siwezi kuacha kuwa makini na vikoba kwa sababu yake. Kama msanii mkubwa tumekuwa marafiki katika mitandao ya kijamii kinyume cha hapo sina muda huo," amesema Giggy.

## Gara B kila kitu kwa mkewe



MSHEREHESHAJI maarufu nchini, Gara B, amesema mke wake anampa pesa ya kuweka sawa uso wake ili kuendelea kuwa kijana.

Akizungumza na EATV, Gara B amesema pale anapoonekana uso wake umechoka kiasi mke wake anamuhimiza kwenda saluni kuweka sawa na kumlipia gharama zote.

"Nakwenda saluni pale mke wangu anaponipatia pesa, nafanya hivyo mara mbili kila baada ya miezi miwili," amesema.



## BABU WA TIK TOK ETI AZEEKI

MWANAMUZIKI mahiri Seif KIsauji, maarufu Babu wa Tik Tok, amesema anabaki kuwa kijana kutokana na kujitunza na kutokuwa na chuki.

Akizungumza hivi karibuni, amesema kuwa kwa sasa amefikisha miaka 60, lakini hadi sasa anaonekana kijana mbichi kutokana na kufuata taratibu mbalimbali ikiwamo kujiweka vizuri, mazoezi na moyo kutokuwa na chuki na wengine.

Amesema watu wengi hasa wasanii wanazeeka haraka kutokana na kupenda sana wanawake na mambo mengine yanayosababisha mwili kuchoka.



## Harmonize, Nandy wapo juu

WANAMUZIKI nyota katika muziki wa Bongo Fleva, Harmonize na Nandy, wamefanya maajabu baada ya kibao chao kipya 'Usemi Sina' kusikilizwa na watu ndani ya saa chache tangu utambulishwe.

Wimbo huo ambao uliachiwa jana jioni kwenye mtandao wa You Tube, ulifikisha watu karibu milioni mbili waliouangalia ndani ya saa tatu pekee.

Mpaka kufikia jana jioni wafuasi zaidi ya milioni tatu wameutazama na kuwa moja ya wimbo uliofanya vizuri katika mtandao huo kwa siku za hivi karibuni.

## KULIA MAGITAA, KUSHOTO BUNDUKI

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI wa utawala wa Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye siku chache zilizopita nchi ilikuwa na kumbukizi ya miaka 25 tangu alipofariki, Mashirika mengi ya umma na kampuni zilikuwa na bendi za muziki wa dansi, taarabu au vyote kwa pamoja.

Na bendi za muziki wa dansi hazikuwa kwenye mashirika na makampuni peke yake, bali hata kwenye majeshi yetu ya ulinzi na usalama.

Leo tutaziangazia bendi za majeshi ya Tanzania. Lengo lilikuwa ni kuwaburudisha makamanda wapiganaji kila wikiendi, wakati mwingine na familia zao.

Kama vile haitoshi, ilikuwa ni kuwapa burudani Watanzania wote, kwani bendi hizo mbali na kupiga makambini, lakini zilikuwa zikipiga kwenye kumbi mbalimbali nchini na zilikuwa zikisafiri nchi nzima.

Kiufupi hazikuwa bendi za mchezo mchezo, kwani zilikuwa maarufu na tishio kwa bendi za raia. Ingawa nyingi bado zipo, lakini si shindani tena kama zamani.

### Mwenge Jazz Band

Hii ndiyo unaweza kusema kama bendi mama ya zote zilizomilikuwa na majeshi. Wenyewe walipenda kuiita 'Mwenge ya Mashujaa'.

Ilikuwa ni bendi tishio na maarufu zaidi ya bendi zote, ikikusanya wanamuziki mahiri nchini Tanzania. Ilikusanya vijana wa Kitanzania wenye vipaji na kuwapa ajira za muziki na jeshi pia.

Hata hivyo kuna wengine walibakiwa kuwa wanamuziki tu. Bendi hii ipo mpaka sasa, ingawa haina nguvu zile kama za mwanzo ilipokuwa ikishindana na bendi kubwa kama za Msondo na Sikinde.

Inamilikiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ). Ilivuma sana katikati ya miaka ya 1970 hadi katikati ya miaka ya 1980.

Nyimbo ambazo zilitia fora na kuifanya bendi hiyo kuheshimika ndani na nje ya nchini ni 'Rehemu', 'Kupa...a kwa Mwezi', 'Mwanahawa', 'Tofali la Barafu','Chenga bin Uto...', na nyingine nyingi.

### Polisi Jazz Band

Ilikuwa ni bendi ya pili kwa ukubwa na umaarufu kwa bendi za majeshi, ukiondoa Mwenge Jazz Band.

Hii inamilikiwa na Jeshi la Polisi la Tanzania, Makao Makuu yake yakiwa maeneo ya Kilwa Road, maeneo ya Kurasini jijini Dar es Salaam.

Iliwika sana miaka ya 1978, hadi 1981 wakati ilipokuwa na wanamuziki mahiri kama Tx Moshi William, Kassim Mapili, Jalala Ally na wengineo. Ilipendwa mno na mashabiki wa muziki wa dansi Tanzania kwa vibao vyao kama 'Tuli', 'Mwaka wa Watoto', 'Mayasa', 'Wivu Sina' na nyingine nyingi. Badu... po, ingawa imepungua makali yake.

### Magereza Jazz Band

Ni bendi inayomilikiwa na Jeshi la Magereza. Haikuwa maarufu sana kuliko zingine. Lakini kuna wakati ilikuwa ikitoa nyimbo chache zilizopendwa.

Hata hivyo, bendi hii ilijinyakulia umaarufu wa muda mfupi, ilipowachukua wanamuziki kama Abel Bathazar, Hassan Kunyata, Nana Njige na wengineo mwanzoni mwa miaka mwanzoni mwa 1990 na mtindo wao wa 'Mkote Ngoma, Kubali Yaishe' na kutoa vibao vilivyoondokea kuwa gumzo kama 'Edina', 'Ashura' na nyingine nyingi.

### JKT Kimbunga Stereo

Bendi hii ilikuwa ya kawaida, lakini ilipomchukua John Simon kutoka Nuta Jazz, ndipo ilipoanza kupiga muziki wa ushindani.

Iliwaleta baadhi ya wanamuziki kama Mwarami Said ambaye baadaye alikwenda Sikinde, na kutoa vibao kama 'Cheza Rhumba Kimbunga', 'Ushirikina', 'Chakula Cha Shida' na nyinginezo.

Bendi hii ilimilikiwa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

### JKT Mafinga 'Kimulimuli'

Pia bendi hii ilimilikiwa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), lakini haikuwa Dar es Salaam, bali mkoani Iringa. Ilikuwa ni kama kikosi cha pili cha JKT Kimbunga. Ni kwamba baadhi ya wanamuziki walioonekana wamekosa nafasi Kimbunga, walipelekwa Iringa. Walimpata pia Zahir Ally Zorro wakafanya kazi ya maana. Wimbo wao wa kwanza ambao uliwafanya kuanza kuwa maarufu na bendi tishio si kwa JKT Kibunga yenyewe tu, bali hata bendi nyingine ni 'Christina' uliotoka mwaka 1977, uliotungwa na kuimbwa na Zahir.

FILAMU

## Chozi la aibu halina huzuni

**Na Adam Fungamwango**

CHOZI la aibu ni filamu inayozungumzia juu ya mama mmoja aliyeachiwa mali na watoto na marehemu mumewe na mke mwenzake. Lakini akaona mali ni kitu chenye thamani zaidi kuliko watoto. Walikuwa ni watoto wa mke mwenzake. Tena wote wawili aliwaua yeye mwenyewe ili apate mali hizo, lakini waswahili wanasema 'muda ni mwalimu mzuri.'

Ni filamu yenye mafundisho mazuri kwa jamii, kwani wapo watu ambao hufikiria mali zaidi kuliko utu. Wanaweza hata kuua ili kupata mali. Mtu anaweza kumuua mumewe, mkewe, baba au mama ili tu arithi mali. Haya yapo sana kwenye jamii.

Imechezwa na Aisha Hamisi kama Suzan, Salma Maneno kama Salma, Juma Ally aliyecheza kama Mbayu, Edward Sanga yeye alivaa uhusika wa Shiko, Kasele Ramadhani kama Shaka.

Inaanza kuonyesha Shaka anaumwa. Yuko hoi bin taaban. Anatoa usia kwa rafiki yake Shiko, akifa mali zake zigawanywe kwa mkewe mkubwa ambaye ana watoto wawili, pia ni mjamzito. Mkewe mdogo ambaye hajabahatika kupata mtoto naye pia apate mali yake. Akafariki dunia. Kifo hicho kumbe kilisababishwa na mke mdogo. Alimuua mumewe kwa dawa za kienyeji ili apate mali. Baada ya kifo cha Shaka, zamu ikawa kwa mke mwenzake. Huyu hakuuawa kwa dawa. Alijifanya amempeleka kliniki, walipofika njiani porini, alimpiga na gongo kichwani na tumboni, akafa pale pale. Suzan akabaki na watoto wawili wa mke mwenzake, Mbayu na Salma. Akaanza kuwatesa. Wakateseka hadi majirani wakaja juu. Hilo halikuwa tatizo kwa Suzan, mwisho akawafukuza kabisa nyumbani.

Katika kutembeatembea wakachukuliwa na baba mmoja, akawapeleka kwa mkewe ili awalee.

Mzee aliwalea kwa mapenzi mema na mkewe hadi walipokuwa wakubwa, wakaenda mjini kutafuta maisha. Maisha yaliwakubali. Hawakusahau kwao. Walirejea na kumkuta mama yao aliyewalea amefariki, lakini baba yao yupo. Walirudisha fadhila kwa mzee yule. Wakaamua kupitia kwa mama yao wa kambo aliyenyanyasa na kuwafukuza. Walimkuta hoi. Anaumwa na hana wa kumtibia. Pia amezeeka sana. Mbayu aliamua kumchukua kumpeleka mjini ili apate matibabu anayostahili. Salma alikataa. Mbayu alimpeleka mjini, akamtibia na kupona. Yeye akasema halipi kisasi kwa yote yaliyotokea. Salma bado alikuwa na kinyongo. Hata hivyo mama alianguka chini ya miguu yake. Akaomba msamaha na kudai kuwa ujana na tamaa ya mali ndiyo vilimfanya awe vile. Hatimaye Salma anamsamehe.



# Ali Baba asimulia siku za mwisho za Abacha



MCHEKESHAJI kutoka Nigeria Ali Baba amesimulia tukio la kustaajabisha katika maisha yake, akieleza alikutana na rais wa zamani wa nchi hiyo, Sani Abacha saa chache kabla ya kifo chake.

Amesema anakumbuka alialikwa katika hafla moja katika kunogesha ambayo kiongozi huyo alikuwapo na kwamba baada ya tukio hilo alisikia amefariki dunia.

"Ulikuwa mkutano wa kwanza kuwa karibu na Sani Abacha, ulikuwa usiku mgumu kutokana na tabia yake isiyotabirika, lakini tulipomaliza tulipata habari ngumu kuwa kiongozi wetu amefariki," amesema Ali Baba.



## Cardi B atangaza vita

RAPA maarufu wa Marekani, Cardi B ametangaza kumchukulia hatua za kisheria mtu aliyehusika kutoa taarifa feki za kuwanyanyasa watoto wake.

Cardi B amesema mtu huyo aliwapigia simu maofisa wa Shirika la Huduma za Kinga ya Mtoto (CPS), na kusababisha kuivamia nyumba yake bila sababu.

Akiwa amekasirishwa na kitendo hicho, rapa huyo alisema kabla ya tukio hilo alikuwa amelazwa hospitalini na alipofika nyumbani kwake alikutana na kadhia hiyo.

## Mtoto wa Diddy amtetea baba yake

MWEZI mmoja baada ya rapa wa Marekani, Sean 'Diddy' Combs kukamatwa kutokana na kukabiliwa na makosa ya biashara ya ngono, utekaji nyara na ulaghai, mtoto wake mkubwa ameibuka na kumtetea kuwa hana hatia.

Quincy akizungumza kwa niaba ya ndugu zake kupitia ukurasa wake wa Instagram, amesema familia yao iko katika wakati mgumu, lakini wanaamini baba yao atashinda mashtaka yote yanayomkabili.

"Mwezi uliopita umekuwa mbaya kwa familia yetu. Wengi wametuhukumu kwa msingi wa shutuma, nadharia za njama na simulizi za uwongo kwenye mitandao ya kijamii. Tunasimama kwa umoja, kukuunga mkono baba kwa kila hatua. Tunashikilia ukweli, tukijua kuwa utashinda, na hakuna kitakachovunja nguvu ya familia yetu," ameandika Quincy.





## Wanigeria wamjia juu Druski

Raia wa Nigeria wamekuja juu baada ya mwigizaji kutoka Marekani Druski, kutoa filamu ambayo inawaonyesha Wanigeria kama watu walaghai wa Kiafrika.

Filamu hiyo ya mchezo wa kuteleza ilichezwa na Druski, imepewa jina la 'Walaghai wa Kiafrika wanaoishi maisha bora zaidi,' na kumwonyesha Mnigeria Baba Oluwatosin akijipatia pesa kwa utapeli.

Katika filamu hiyo inaonyesha matumizi ya Naira na kadi nyingi za ATM za Nigeria.

## Timaya kama Portable vile

MWANAMUZIKI wa Nigeria Timaya, amesema amevutiwa na msanii mwenzake Portable, kwa sababu tabia zao zinaendana.

Akizungumza hivi karibuni, Timaya amesema alikumbuka mara ya kwanza aliposikia nyimbo za Portable na hapo alifahamu kuwa wanafanana kuwa na tabia zenye utata.

"Ndiyo maana nampenda Portable, mara ya kwanza alipotoka, nilimweleza 2face kuhusu yeye. Tukiwa njiani kuelekea Jimbo la Delta nikamwambia, je, umemsikia mtu huyu anaitwa Portable?' Huyo jamaa ni kama mimi kwa sababu tupo kama vichaa." Amesema.





## HABARI KASKAZINI

# Serikali kuifufua Tazara kuimarisha usafiri wa reli

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WAZIRI wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema serikali iko mbioni kufufua Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), ili kuimarisha usafiri wa reli unaounganisha Bandari ya Dar es Salaam na nchi za Kusini mwa Afrika hususani za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Aidha ameliagiza Shirika la Reli Tanzania (TRC) kushirikiana na sekta binafsi kuhakikisha inaimarika zaidi katika kuleta mapinduzi kupitia sekta ya usafirishaji.

Prof. Mbarawa aliyasema hayo jana katika kikao cha 17 cha mkutano wa mapitio ya utendaji kazi cha uchukuzi kwa mwaka 2024 na kuongeza kuwa reli ya TAZARA ni njia muhimu kwa uchumi wa nchi kutokana na kuunganisha Dar es Salaam na mataifa ya SADC kupitia usafirishaji wa mizigo.

Alisema reli ya TAZARA ilianza kujengwa mwaka 1970 na kukamilika mwaka 1975, ikiwa na urefu wa kilometa 1,860 na ilijengwa kwa mfumo maalum wenye kulenga kuimarisha uhusiano wa kiuchumi kati ya Tanzania na nchi jirani.

Prof. Mbarawa alisema kufufuliwa kwa TAZARA ni hatua muhimu kwa uchumi wa nchi zote zinazotumia reli hiyo, kwani awali reli hiyo ilibuniwa kubeba mizigo yenye uzito wa tani milioni 5.5 kwa mwaka, lakini lengo hilo halijawahi kufikiwa. Mwaka 1986, TAZARA ilisafirisha tani milioni 1.2 ikiwa ni kiwango cha juu zaidi kilichowahi kufikiwa.

"Ufufuaji wa reli hii utahusisha pia uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam endapo reli itafikia uwezo wa kusafirisha tani milioni mbili kwa mwaka, mapato ya Bandari ya Dar es Salaam yataongezeka kwa kiasi kikubwa na kuifanya Tanzania kujipatia fedha nyingi zaidi," alisema.

Ufufuaji wa reli ya TAZARA ni hatua muhimu si tu kwa Tanzania na Zambia, bali kwa nchi zote za Kusini mwa Afrika, kwani mradi huo unalenga kuimarisha usafirishaji wa mizigo, kukuza uchumi wa kikanda, na kuongeza mapato kwa nchi zinazohusishwa.

"Serikali inaamini kupitia ushirikiano huu mpya, reli ya TAZARA itarejea kwenye ufanisi wake wa awali na kuwa chombo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi ya eneo hili lakini pia TRC iongeze nguvu zaidi katika ushirikiano na sekta binafsi ili kukuza uchumi," alisema. Kuhusu umuhimu wa Reli ya Kisasa ya SGR alisema teknolojia inakuwa kwa kasi kubwa hivi sasa, SGR unatoka Dar es Salaam hadi Dodoma ambapo zamani watu walikuwa wakitumia saa tisa sasa hivi saa tatu kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma na hayo ndio maendeleo makubwa yanayopaswa kupongezwa na kujivunia kwa kila Mtanzania.

"Ni muhimu TRC kushirikiana na sekta binafsi katika kukuza uchumi kwani serikali imebadilisha sera na kanuni za uwekezaji sababu tunataka Watanzania kushirikiana na sekta binafsi katika kuleta maendeleo zaidi," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara, alisema wizara hiyo inafanya jitihada za kupunguza msongamano wa magari katika miji mikubwa nchini, ikiwamo Dar es Salaam na Dodoma kwenda Mashariki ya Dar es Salaam, kwa kutumia barabara ya mwendokasi ikiwamo kuboresha na kuweka mpangilio mzuri wa malori yanapotoka na kuingia bandarini.




Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Salim Msangi (wa pili kulia), alipotembelea banda la mamlaka hiyo, katika Mkutano wa 17 wa Wadau wa Sekta ya Uchukuzi kuhusu Ufuatiliaji na Tathmini, jijini Arusha juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara waonywa ukwepaji kodi

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, ameagiza wafanyabiashara ambao wameshatambuliwa kuwa walipakodi wasisubiri kusukumwa bali walipe kodi badala ya kukwepa.

Kigahe alitoa agizo hilo jana mjini hapa wakati akifungua maonesho ya Tanzanite Manyara Fair 2024 yaliyoandaliwa na Chama cha Wafanyabiashara, Kilimo na Wenye Viwanda (TCCIA) mkoani Manyara chini ya ufadhili wa Kampuni ya Mati Super Brands Limited.

Alisema kama bidhaa ya mfanyabiashara haina nembo ya ubora hawezi kwenda nchi za Afrika Mashariki na kufanya biashara.

"Walipakodi ambao tumeishatambulika tulipe kodi tusikwepe na tutoe risiti za EFD maana nyie ndio wakala wa serikali wa kukusanya mapato," alisema Kigae.

Aidha, alisema ni vizuri wakalipa kodi fedha hiyo ongezeko la thamani (VAT) asilimia 18 si wao wanailipa bali ni mtumiaji wa mwisho hivyo waache kuogopa.

Kuhusu maonesho hayo alisema yanasaidia watu kujifunza na mkoa wa Manyara ni eneo la kimkakati hivyo watu wakiwekeza ni rahisi kusafirisha bidhaa zao.

Kigahe alisema serikali itaendelea kutunga sera za kuwavutia wawekezaji na wameweza kuhuisha sera ya biashara na wataendelea kuboresha sera na kutunga sera zinazoendana na wakati wa sasa.

Alitumia fursa hiyo kuionya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) kuacha kugonganisha ratiba za maonesho kwa kuwa kufanya hivyo ni kuwanyima watu fursa ya kushiriki na viongozi kushindwa kufika.

"Mgongano wa maonesho hili halikubaliki na lisijirudie hawa ndio wanatoa kibali cha kufanyika iweje maonesho yagongane leo," alisema Kigahe.

Alisema TANTRADE ndio inatakiwa kuhakikisha maonesho yanatakuwa na tija na wahusika wasigombane ili wapate fursa ya kushiriki.

Naye mfadhili wa maonesho hayo kutoka Kampuni ya Mati Super Brands Limited, Ngwandumi Mpoma, akitoa maelezo ya bidhaa zinazozalishwa na kampuni yake alisema wameajiri vijana 312 na wamefadhili mfululizo wa maonesho miaka mitatu.

Mpoma alisema licha ya kutoa ufadhili huo bado mwamko wa wenyeji ni mdogo sana awamu ijayo wanahitaji wawe wengi sana ili wafanyabiashara waweze kunufaika.

Akizungumza Katibu Mtendaji wa TCCIA mkoani hapa, Zainab Rajab, alisema bado wana tatizo la uongezaji wa thamani kwenye bidhaa zao.

Rajab alisema wanaishukuru serikali kwa kuendelea kuunga mkono jitihada za wafanyabiashara. Makamu wa Rais wa TCCIA, Boniface Ndengo, aliomba serikali kurasimisha wajasiriamali wadogo na wabunifu, wizara ya viwanda na biashara kuwapatia maeneo maalumu ya maonesho kila mkoa ili kuepuka kuhamisha vitu na wanataka wajenge makampuni makubwa ya kimkakati.

Mkuu wa Wilaya ya Babati, Emmanuela Kaganda, akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, alisema mkoa huo una viwanda 200 ila vingi ni vidogo bado wana uhitaji wa viwanda vikubwa kwa kuwa malighafi zipo za kutosha.

## Kikwazo cha ajira kwa wenye ulemavu chatajwa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KUTOKUKUMBUKWA katika ajira kwa watu wenye ulemavu wa macho kutokana na kutokufuatwa kwa Sheria ya Ajira kwa Watu Wenye Ulemavu ni tatizo kubwa linaloikumba jamii, imeelezwa.

Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye Ulemavu wa Macho Tanzania (TLB), Habiba Salum, alisema hayo wakati akizungumza katika kongamano la fimbo nyeupe kuelekea kilele cha maadhimisho ya miaka 60 tangu kuanzishwa kwa chama hicho lililofanyika ukumbi wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro.

Alisema wako wenye ulemavu wa kutokuona ambao wamesoma na wanavyeti vyao bali ajira hawana hivyo niombe serikali iangalie wakati inapofanya usaili iangalie kundi hili.

"Tatizo linalotukabili kwa wingi sisi wenye ulemavu wa macho ni ajira katika kada yetu. Wako wasomi wengi na wana vyeti vyao lakini hawajapata ajira. Naiomba serikali wakati huu inafanya usahili kwa ajili ya kuwapata wafanyakazi waiangalie kada hii.

"Kama sikosei iko sheria inayoelekeza asilimia tatu ya ajira ni kwa watu wenye ulemavu ingawa serikali inajitahidi bado katika sekta binafsi jambo hili halizingatiwi kama wangetimiza tatizo la ajira lisingekuwa kubwa," alisema.

Mwenyekiti huyo pia alisema bado jamii inakabiliwa na tatizo la unyanyapaa kwa watu wenye ulemavu kwa kuwafungia ndani na kuwanyima huduma za kijamii.

Wakati huo huo, mwenyekiti huyo alisema kongamano hilo watalitumia kuwahamasisha wananchi kutambua watu wenye ulemavu wa macho ni wa aina gani na wanamahitaji ya aina gani lakini pia madereva waweze kutambua fimbo nyeupe inamaana gani.

Akifungua kongamano hilo, Mratibu wa Chama cha Wasioona Tanzania (TLB), Kizito Wambura, aliwaonya watu ambao wamekuwa wakiwatumia watu wenye ulemavu wa macho kujipatia kipato kuacha tabia hiyo kwa kuwa ni kosa kwa mujibu wa sheria na yeyote atakayebainika kufanya hivyo atafikishwa mahakamani.

Wambura alisema kongamano hilo pia litatumika kutoa maoni yao kwa ajili ya kuhuisha Sera ya Taifa ya Watu Wenye Ulemavu wa Macho ambayo ilitungwa mwaka 2004 na ni muda mrefu umepita hivyo inahitaji kufanyiwa mapitio.

Mmoja wa washiriki wa kongamano hilo, Mwalimu Mussa Mashauri, alisema mtazamo wa jamii kwa watu wenye ulemavu wa wasioona si mzuri huku pia suala la umaskini likitajwa kama kikwazo kwa jamii ya watu wenye ulemavu wa macho.

MAKALA

TULIKOTOKA,TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Marijani alipokacha ukipa Simba, na kuwa mwanamuziki maarufu

**Na Adam Fungamwango**

HUU ni mwaka wa 29 tangu Tanzania ilipompoteza mmoja wa wanamuziki bora kabisa waliowahi kutokea, Marijani Rajab.

Machi 23, mwaka huu, Tanzania iliadhimisha miaka 27 ya kifo cha mwanamuziki maarufu, aliyelitangaza jina la nchi nje ya mipaka, Majirani Rajab.

Alifariki nyumbani kwake Kariakoo Mtaa wa Somali, Machi 23, 1995, karibu kabisa na maeneo ya Gerezani, na kuzikwa kesho yake kwenye makaburi ya Kisutu, Dar es Salaam.

Hadi leo, Marijani anabaki kuwa mmoja wa wanamuziki wachache nchini ambaye bado ameendelea kuwa maarufu kizazi hadi kizazi hata baada ya kufariki.

Ni mwanamuziki aliyeimba nyimbo za maudhui yote. Siasa, mapenzi, matukio, ukombozi barani Afrika, matatizo ya kijamii na mengine mengi.

Alitunga na kuimba zaidi ya nyimbo mia tatu hadi kufariki kwake. Baadhi ya nyimbo ambazo ni maarufu zaidi hadi leo hii na zingine zimerudiwa na wasanii wa kizazi kipya ni 'Zuwena', 'Mwanameka', 'Siwema', na nyingine nyingi, kwani ukiziorodhesha nyimbo zake hapa, unaweza kujaza ukurasa mzima.

Kutokana na kazi zake nyingi na umaarufu wa mwanamuziki huyo, aliyepachikwa jina la 'Jabali la Muziki', unaweza kudhani kuwa alifariki dunia akiwa na umri mkubwa sana. La hasha. Alifariki akiwa na miaka 40 tu. Alizaliwa Machi 3, 1955 na kufariki Machi 23, 1995 na kuacha vilio, simanzi na huzuni kwa mashabiki wa muziki wa dansi nchini.

Marijani alianza muziki akiwa bado mdogo sana akiwa anasoma, kitu ambacho kilimletea matatizo yeye mwenyewe na bendi ambazo amepigiwa mwanzo kama tutakavyoona baadaye, lakini si wengi wanaojua kuwa alikuwa na kipaji kingine cha kucheza soka.

Alikuwa golikipa mahiri wa Shule ya Sekondari ya Kinondoni Muslim, baadaye akaibukia Tambaza alipokuwa akisoma, huku pia akipiga muziki, lakini mitaani alikuwa akidakia timu mbalimbali, huku timu yake kubwa ikiwa na Kahe FC.

Umahiri wake ulimfanya aanze kuwindwa na klabu ya Simba kwenda kuidakia, huku mwenyewe akiwa na mpenzi wa klabu hiyo na alikubali.



Kwa mujibu wake mwenyewe wakati wa uhai wake akihojiwa, alisema hakwenda Simba kwa sababu tayari alishachagua muziki kama ni kazi yake halisi badala ya mpira, kwani awali alikuwa hajui aende wapi kati ya muziki na mpira, huku vitu vyote viwili akivifanya kwa uwezo sawa.

Marijani aliweza kutoka nje ya Tanzania kwa mara ya kwanza ambapo alikwenda Nairobi na kurekodi nyimbo zilizotoka katika lebo ya Phillips. Hili jambo la mwanafunzi kusafiri na bendi likaleta shida na kwa vile (STC) ilikuwa mali ya umma, akatimuliwa mwaka 1972, lakini alijiunga na Safari Trippers ya David Mussa ambayo kwa wakati huo ilikuwa inapiga zaidi nyimbo za hoteli na za kukopi na muimbaji wao kiongozi wakati huo alikuwa Ali Rajabu.

Hapa ndipo ubora wake ulifunguka haswa na kuweza kuinyanyua Trippers, kwani waliweza kutoa vibao vilivyopendwa mfululizo na kuweza kuzunguka nchi nzima. Vibao kama Rosa Nenda Shule, Georgina, Mkuki Moyoni, viliweza kuuza zaidi ya nakala 10,000 za santuri na hivyo kuwezesha bendi kuwa na vyombo vyake vizuri.

Mwaka 1976, Marijani na baadhi ya wanamuziki wa Trippers waliamua kuihama bendi na kwenda baadaye kuasisi Dar es Salaam International chini ya umiliki wa Mzee Zakaria Ndabemeye. Baadhi ya wanamuziki hao ni pamoja na Abel Baltazar kutoka Msondo, Kassimu Mponda kutoka Trippers, Abdallah Gama, Joseph Mulenga, Haruna Lwali na George Kessy Omojo waliokuwa wanapiga muziki Magot pale, Said Mohamed kutoka Polisi Jazz, Cosmas Chidumule kutoka Urafiki, Belesa Kakere kutoka Biashara Jazz, Joseph Bernard kutoka Trippers, Ali Rajabu kutoka Trippers, na King Michael Enock kutoka Dar es Salaam Jazz.

Akiwa Dar Inter alishiriki kutunga nyimbo mbili, Betty na Sikitiko. Hata hivyo kama waswahili wanavyosema mafahari wawili hawakai zizi moja ndivyo ilivyotokea kati yake na Abel Balthazal kiasi cha hatimaye Marijani kufukuzwa ndani ya bendi kutokana na ubishi kuhusu wimbo aliotunga Marijani, kuna maelezo kuwa wimbo ulionekana unafanana na wimbo fulani toka Kongo na hivyo Marijani akatakiwa aubadilishe na ndipo ugomvi ukaanza.

Hata hivyo mwishoni mwa mwaka 1978, Marijani alirejeshwa tena kundini kutokana na rundo la wanamuziki wa Dar Inter kuihama bendi kwa kishindo kikubwa na kwenda kuifungua bendi mpya kabisa ya Orchestra Mlimani Park. Aliporejeshwa Marijani alikuja na wanamuziki wengi wapya wakati huo kama akina Christopher Kasongo, Mohamed Tungwa, Mafumu Bilal, Hamis Milambo, Athuman Momba, Mzee Alex Kanyimbo na wengine na kuja na mtindo wa Super Bomboka.

Katika kudhihirisha hasira zake kwa Abel, Marijani alimtungia Abel wimbo wa 'Kidudu Mtu' ambao hata hivyo RTD waliukataa kuurekodi, jambo lililokuwa kawaida enzi hizo kwa redio kukataa nyimbo. Wanamuziki wengine aliohamia ni Fresh Jumbe, Mohamed Mwinyikondo, Juma Choma, Tino Masinge na wengineo.

Hata hivyo safari ya Dar International ilikoma mwaka 1987 kutokana na sababu za kawaida za kufa kwa bendi lakini kubwa ni uchakavu wa vyombo. Hata hivyo Marijani aliendelea kufanya muziki na kwa kipindi kifupi amewahi kucheza na Kurugenzi ya Arusha na Mwenge Jazz ambayo alirekodi nayo wimbo mmoja wa Ukimwi na hata kupitia bendi ya Watafiti.

Aidha mwaka 1994 aliwahi kurekodi 'zong zing' na marehemu Eddy Sheggy.

Bendi yake ya mwisho ilikuwa ni Africulture ama Mahepe Ngoma ya Wajanja, iliyokuwa mali ya Rogers Malila, alikokuwa na wanamuziki kadhaa kama akina Hassan Kunyata, Mgosi na wengine. Bado Marijani ataendelea kukumbukwa na wapenda muziki kote nchini na hata Afrika kwa ujumla kwa nyimbo zake tamu na zenye mafundisho.



Marijani Rajab

## Marekani haitaki vita Lebanon

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imesema haitaki vita vinavyoendelea Lebanon kuwa vya muda mrefu.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, alisema hayo wakati akitoa ripoti kuhusu juhudi za kufanya mazungumzo mapya kuhusu makubaliano ya kusitisha mapigano na mpango wa kuachiliwa kwa mateka wanaoshikiliwa na Hamasi katika Ukanda wa Gaza.

Blinken alisema mwezi mmoja baada ya mashambulizi ya kijeshi yanayofanywa na Israel dhidi ya kundi la Hezbollah nchini Lebanon anatumai Iran inapata ujumbe wa wazi kwamba mashambulizi yoyote zaidi dhidi ya Israel yanahatarisha maslahi yake.

Israel iliapa kulipiza kisasi baada ya shambulio la kombora la Iran mnamo Oktoba 1, mwaka huu.

Mkuu wa Jeshi la Israel alisema kumalizika kwa mzozo na Hezbollah kunawezekana lakini hakutoa maelezo zaidi.

Mashambulizi kadhaa ya Jeshi la Israeli yalilenga viunga vya kusini mwa Beirut jioni ya Alhamisi.

Hata hivyo, wapatanishi wa Israel na Hamas watakutana mjini Doha kujiandaa kwa mazungumzo mapya kuhusu makubaliano ya kusitisha mapigano Gaza ambayo yatahusisha pia kuachiliwa kwa mateka wanaoshikiliwa katika eneo la Palestina la Gaza.

Aidha, Israel ilisema mkuu wake wa shirika la kijasusi la Mossad David Barnea, atasafiri hadi Doha Jumapili ya wiki hii kujaribu kuanzisha upya mazungumzo, na kukutana na Mkurugenzi wa CIA, William Burns na waziri mkuu wa Qatar. “Pande zote zitajadili hatua mbalimbali za kuanza mazungumzo ya kuachiliwa kwa mateka kutoka kwa Hamas, licha hali ilivyo kwa sasa,” ofisi ya Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu ilisema.

**BBC**

# Putin aiachia Marekani hatima ya uhusiano wao

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia, Vladimir Putin amesema uhusiano kati ya nchi yake na Marekani utategemea mtazamo wa serikali itakayoingia madarakani.

Akitoa maoni yake kuhusu uchaguzi wa Marekani, kiongozi huyo aliyapongeza maoni ya mgombea wa Republican, Donald Trump, kuhusu kumaliza vita vya Ukraine.

Rais Putin aliyasema hayo wakati mgogoro kati ya nchi yake na Ukraine ukizidi kufukuta.

Akizungumza mbele ya waandishi wa habari, Putin alisema mtazamo na msimamo wa serikali ya Marekani juu ya Russia baada ya uchaguzi mkuu wa nchi hiyo utakaofanyika mwezi Novemba utaamua hatima ya uhusiano wa nchi hizo mbili.

“Jinsi uhusiano wa Russia na Marekani utakavyokuwa baada ya uchaguzi itategemea Marekani yenyewe wakiwa wawazi, basi na sisi pia tutakuwa wazi. Na ikiwa hawataki, basi sawa. Hili ni juu ya utawala ujao wa nchi hiyo utakavyochagua,” alisema Putin.

Rais Putin aliunga mkono maoni yaliyotolewa na rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump ambaye anawania urais wa Marekani katika uchaguzi ujao kuhusu nia yake ya kuvimaliza vita lakini ikiwa tu msimamo huo utakuwa wa dhati.

Katika hatua nyingine, maofisa wa mji mkuu wa Ukraine, Kiyv, walisema mapema jana kuwa Russia imefanya mashambulizi ya anga usiku kucha.

Msimamizi wa jeshi katika mji huo, Serhiy Popko alisema katika mtandao wa Telegram kuwa droni kadhaa zilidunguliwa katika mashambulizi hayo.

Msimamizi huyo ameongeza kuwa mpaka sasa mamlaka hazijapokea taarifa zozote juu ya uharibifu au majeruhi kutokana na mashambulizi hayo.

Waandishi wa habari wa Reuters waliripoti kusikia milipuko mingi jana, huku jeshi la anga la Ukraine likisema katika taarifa yake kwamba ulinzi wake wa anga uliziharibu droni 36 kati ya 63 zilizorushwa usiku kucha na Russia.

**DW**



Baba na mtoto wake wakiwa wamejihifadhi kwenye mabaki ya nyumba yao, iliyoporomoshwa na mabomu ya Israel katika kitongoji cha Khan Younis jana. **PICHA: REUTERS**

# Wakenya wasimamisha mtandao wa seneti

**NAIROBI,** KENYA

BUNGE la Seneti la Kenya limethibitisha kutokea matatizo ya kiufundi na mfumo wao wa barua pepe kufuatia wimbi la mawasilisho yaliyotolewa na raia kuhusu muswada wa kubadilisha katiba.

Muswada huo, uliowasilishwa na seneta wa Nandi, Samson Cherargei, unalenga kuongeza ukomo wa muhula wa Rais, Magavana, na wabunge wa bunge la taifa na wawakilishi wa mabunge ya kaunti kutoka miaka mitano hadi saba.

Kipindi cha utoaji maoni kwa umma kuhusu muswada huo, kilimalizika jana, huku Wakenya wakitakiwa kutoa maoni yao kwa njia ya mkono katika Ofisi za Seneti, au kwa barua pepe.

Kongamano la ushiriki wa umma linalojadili muswada huo kwa sasa linafanyika katika ukumbi wa KICC, jijini Nairobi, ambalo linakusanya maoni ya Wakenya. Mswada huo unakabiliwa na ukosoaji kwa watu wa kada mbalimbali. Baadhi ya Wakenya walieleza masikitiko yao kuhusu mtazamo wa serikali wa kutosikia katika kutekeleza majukumu yake. Kulingana na Seneti, mfumo wao wa barua pepe umepokea zaidi ya mawasilisho 200,000, na kufikia upeo wa juu wa anwani za barua pepe.

**BBC**

# Venezuela yaikosoa Brazil kujiunga BRICS

**CARACAS,** VENEZUELA

VENEZUELA imekosoa uamuzi wa Brazil wa kupinga kujiunga katika kundi linaloinukia kiuchumi la Brics.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Venezuela, ilieleza hatua hiyo ni kama uchokozi.

Uhusiano kati ya serikali hizo mbili umezidi kuwa mbaya tangu kufanyika kwa uchaguzi wa Rais wa Venezuela Julai mwaka huu. Rais Nicolás Maduro alisema amepata ushindi katika uchaguzi huo, licha ya ushahidi kwamba kiongozi wa upinzani Edmundo González, alipata kura nyingi.

Rais wa Brazil Luiz Inacio Lula da Silva ambaye alimuunga mkono Maduro, kwa sasa amegeuka na kukataa matokeo hadi mchanganuo wa kura utakapotolewa. Venezuela ilishawishi kujiunga na Brics, na Maduro alihudhuria kwa kushtukiza katika mkutano wa kilele uliofanyika katika jiji la Kazan na kutangaza kuwa nchi yake ni sehemu ya familia ya Brics.

Rais wa Russia, Vladimir Putin, ambaye alikuwa mwenyeji wa mkutano huo, alisema anakubaliana na msimamo wa Venezuela, lakini akaongeza kuwa itaweza kujiunga na Brics ikiwa kutakuwa na maafikiano miongoni mwa wanachama wake.

**DW**

# Absa Tanzania yaahidi huduma bora zaidi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Benki ya Absa Tanzania ikihitimisha wiki ya huduma kwa wateja kwa kukutana na wateja wake katika hafla maalumu jijini Dar es Salaam juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Obedi Laiser, amesema wanatarajia kutoa huduma bora zaidi kwa wateja.

Kwa kukutana na wateja hao, amesema tukio hilo ni ishara ya shukrani kwa wateja wao waaminifu huku ikitambua mchango wao muhimu katika ukuaji na mafanikio ya benki hiyo kwa miaka mingi.

"Wateja wetu ndio moyo wa kila tunachofanya. Hafla hii ya kufungua kinywa ni ishara ndogo ya shukrani yetu kwa imani na uaminifu mliotuonesha. Tumejikita kikamilifu kutimiza ahadi zetu kwa kutarajia na kukidhi mahitaji yenu katika kila hatua.

Msaada wenu wa kuendelea umekuwa msingi wa mafanikio yetu, na tutaendelea kujitahidi kufanya zaidi ya matarajio yenu," alisema Laiser.

Kaulimbiu ya Wiki ya Huduma kwa Wateja ilikuwa 'Above and Beyond', yaani 'Zaidi ya Matarajio' huku akisema inahusiana kwa karibu na kujitolea kwa benki hiyo kuvuka matarajio ya wateja na kutoa huduma bora.

"Katika Absa, tumejikita katika kutoa viwango vya juu vya huduma. Uhakika, ufanisi, faragha na uadilifu ni nguzo kuu zinazotuongoza katika uzoefu wa wateja wetu. Wafanyakazi wetu ndio msingi wa dhamira hii na tunawekeza katika maendeleo yao ili kuhakikisha tunatoa huduma bora kila mara. Tunafanya kazi kama timu moja, tukiwazingatia wateja wetu katika kila tunachofanya," alisema.

Alisisitiza zaidi kwamba benki inajitahidi kutoa huduma makini, inayofika kila mahali na isiyo na makosa, huku ikihakikisha wateja wanapewa taarifa katika kila hatua.

Katika matukio nadra ambayo matarajio ya huduma hayafikiwi, alisema benki inaahidi kurekebisha hali hiyo haraka, ikionesha zaidi msimamo wake wa kuweka wateja mbele.

Kama sehemu ya jitihada za benki hiyo za kuendelea kujihusisha na wateja na kuwazawadia kwa uaminifu wao, Absa Tanzania pia ilitumia fursa hiyo kuwakumbusha watu waliohudhuria kuhusu kampeni yake inayoendelea ya "Spend & Win."

Kampeni hiyo, ambayo iko wazi kwa wateja wote binafsi, inawapa washiriki nafasi ya kushinda Subaru Forester ya mwaka 2014 na zawadi zingine za kusisimua. Droo ya kwanza ilifanyika Oktoba 22, mwaka huu, na benki ilikuwa na furaha kutangaza kuwa mshindi tayari amechaguliwa, huku hafla ya utoaji wa gari ikitarajiwa kufanyika hivi karibuni.

Akihitimisha hafla hiyo, Laiser alisisitiza tena ahadi ya benki hiyo ya kuwawezesha wateja wake na kuhakikisha wanahisi kuthaminiwa katika kila hatua.

"Tutaendelea kusikiliza mahitaji yenu na kutoa suluhisho zitakazowawezesha kufikia malengo yenu ya kifedha. Pamoja, tunajenga Afrika ya kesho pamoja, hatua moja baada ya nyingine," alisema.




Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Tigo Pesa, Arnold Ngarashi (kushoto), akitoa elimu kwa mteja kuhusu huduma ya simu za mkopo katika maadhimisho ya Wiki ya Huduma za kifedha, kwenye viwanja vya Ruanda Nzovwe, jijini Mbeya jana.Maadhimisho hayo yanalenga kuelimisha wananchi kuhusu matumizi ya huduma rasmi za fedha pamoja na kuongeza mchango wa Sekta ya Fedha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madereva 100 wafungiwa leseni kwa makosa usalama barabarani

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi nchini kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani hadi kufikia Oktoba 23, 2024 limefungia leseni za udereva kwa madereva zaidi ya 95 kutokana na makosa mbalimbali ya usalama barabarani ikiwamo mwendokasi.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Naibu Kamishna (DCP) Ramadhan Ng'anzi, alisema hayo juzi wakati akizungumza na madereva na abiria katika Kituo Kikuu cha Mabasi Nyegezi na Nyamhongoro mkoani Mwanza.

DCP Ng'azi alisema licha ya hatua hiyo, watahakikisha wanawachukulia hatua kali za kisheria madereva wote ambao hawatazingatia sheria za usalama barabarani hususani wanaoendesha magari kwa mwendokasi na makosa mengine hatarishi.

Alisema magari yaliyokamatwa yalikuwa na makosa mbalimbali ikiwamo kukosa taa 2,250, yaliyozidisha abiria 4,405, abiria kutokufunga mikanda 30, mabovu 12,000, mwendokasi 5,000 na pikipiki 3,000 huku zaidi ya madereva 40 wakikamatwa kwa ulevi.

Mwenyekiti wa Usalama Barabarani, Ferdinand Chacha, alisema imekuwa desturi kwa madereva wengi wanapoendesha vyombo vya moto kutumia vilevi hali inayochochea ongezeko la ajali barabarani.

Katika hatua nyingine Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kennedy Mgani, alisema mkoani humo wamekamata magari kwa makosa ya usalama barabarani 4,385 pamoja na kumfungia dereva mmoja leseni kwa kipindi cha miezi mitatu, kutokana na kuendesha gari kwa mwendokasi.

Mgani aliviambia vyombo vya habari kuwa kati ya makosa hayo, makosa ya magari ni 3,358, bajaji na pikipiki 1,027 na wahusika waliwajibishwa kwa kulipa faini za papo kwa papo sambamba na mmoja ambaye kufungiwa leseni.

Aidha, alisema katika kipindi hicho walikamata watuhumiwa 14 pamoja na vielelezo mbalimbali, ikiwamo pombe ya moshi lita 87 na mitambo miwili ya kutengeneza pombe hiyo, TV tatu, secoder moja, meza mbili, viti sita vya plastiki, pikipiki sita na gari moja aina ya Scania likisafirisha mazao kinyume cha sheria.

**Imeandaliwa na Marco Maduhu (SHINYANGA), Vitus Audax (MWANZA)**

## Chanzo vikundi kutokurejesha mikopo chatajwa

**Na Elizabeth Seleman, SENGEREMA**

MKUU wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga, amesema moja ya mambo yanayokwamisha urejeshwaji wa mikopo ya asilimia 10 ya halmashauri ni pamoja vikundi vinavyochukua kutokuwa na miradi ya uhakika, hivyo kutaka usimamizi katika utoaji wa mikopo hiyo.

Ngaga alibainisha hayo juzi wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya utoaji na usimamizi wa mikopo ya asilimia 10 kwa maofisa maendeleo ya jamii kata, polisi kata na watendaji kata.

Aliwataka kusimamia vyema vikundi vinavyopatiwa mikopo hiyo itokanayo na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri ili ilete maendeleo na vikundi kuendelea na si kudidimia.

"Vikundi vingi vinavyokopeshwa havifanyi vizuri kutokana na kutokuwa na usimamizi mzuri wa matumizi ya fedha, kusuasua na kutokuwa na miradi yenye uhakika, hivyo niwatake mwende kusimamia vyema vikundi hivyo ili mikopo hiyo itakapoanza kutolewa inufaishe vikundi hivyo," alisema Ngaga.

Mkuu huyo wa wilaya aliwataka maofisa hao kuwa sehemu ya mafanikio ya vikundi hivyo kwa kuwa serikali inatoa fedha nyingi, hivyo wasitoe mikopo kwa watu ambao watatuharibia katika kulifanikisha suala hilo.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Wilbard Badola, alisema wametenga Sh. milioni 436.4 kwa ajili ya kufanikisha mikopo hiyo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu watakaokidhi vigezo vya kupatiwa mkopo.

Alisema kwa kipindi hiki watahakikisha mikopo hiyo inatolewa kwa mujibu wa utaratibu ulioelekezwa na serikali ambao utasaidia kuondoa udanganyifu na urejeshwaji wa mikopo hiyo kwa haraka ili ikopeshwe kwa makundi mengine.

Pia alisema baada ya mafunzo, vikundi vyote vilivyokidhi vigezo vya kupatiwa mkopo vinatakiwa kuanza kutuma maombi ambako mwisho wa kutuma maombi hayo itakuwa ni Novemba 10, mwaka huu na mchakato wa kuyapitia pamoja na taratibu zingine zitaendelea kuhakikisha vikundi vilivyotuma maombi vinakidhi vigezo vya kupata.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.
Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile.
Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosababisha kuwa na tundu kichwani.

# Damu ya Mariamu-35

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Mabosi walishangazwa sana, kwani afande Willy ni mmoja wa maafande vijana, wapole, wanyenyekevu, ambapo hawakudhania kuwa angeweza kuwa na mbinu za kipelelezi za hali ya juu kama zile.

Katika kikao chao walikubaliana kuwa afande huyo anaweza kuwa msaada mkubwa na nchi siku zijazo. Hawakumwambia chochote, bali kumtangaza kuwamo kwenye kundi la kufanya uchunguzi sakata lile na yeye aliwekwa kuwa wa pili baada ya afande mmoja wa juu.

Haukuwa uchunguzi mkubwa, mkali, wa kuvutia na wenye misukosuko kama ule wa kina Kamal na afande Willy.

Ni kwa sababu walikuwa wanarudia tu mle mle. Walikuwa wanapata kila kitu kwa urahisi, tofauti na ule wa mwanzo ambao ulibidi utumiwe mbinu za hali ya juu bila kujulikana.

Wiki moja tu, tayari upelelezi ulikamilika na ushahidi ulipelekwa. Haikutofautiana na ule ulioandikwa gazetini na kwenye televisheni, haukuwa tofauti na ule alioutia Kamal ambao ndiyo huo huo aliwapa waandishi.

Kila kitu kilikuwa wazi. Jeshi la Polisi liliamuru Materu akamatwe, ili akafunguliwe mashtaka ya mauaji, yeye na wenzake wanane ambao walishiriki kwa njia moja ama nyingine, wakiwamo waliomuua Mariamu kwa mkono wao.

Haikuwa rahisi kumkamata mtu tajiri kama Materu. Ilibaki kidogo tu afanikiwe kutoroka nchini. Alikamatiwa Namanga akiwa anataka kuvuka mpaka kuingia nchini Kenya.


Akarudishwa Dar es Salaam na kupelekwa rumande akisubiri kesi yake. Wakati huo Kamal na rafiki yake afande Willy walikuwa wamekaa sebuleni na macho yao walimuona Materu kwenye televisheni akiwa amefungwa pingu akirejeshwa Dar. Wakaangaliana, wakatabasamu. Pamoja na kuwa huru na kufanikiwa kurudi nyumbani kwake, bado Kamal alipendelea kuishi kwa rafiki yake huyo kwani walianza kushibana na kuwa kama rafiki wa damu.

**********************************

Kesi ya Materu na wenzake wanane ilianza kuunguruma kwenye Mahakama Kuu nchini na kufurika watu wengi.

Mamia ya watu walifurika kusikiliza kesi hiyo iliyokuwa na mvuto mkubwa kwenye jamii.

Mvuto wake ulikuwa mkubwa kutokana kwanza na kuuawa kwa msichana mrembo ambapo hata magazeti yalipotoa picha yake na video zake fupi, kila mmoja hata wanawake walikubali kuwa alikuwa mmoja wa wanawake warembo mno kuwahi kuwaona.




**"Ingawa tumeapa kutotengena nawe mpaka kifo kabla hata hatujafunga ndoa, lakini inatubidi tutengane, niwaridhishe wale wabaya kwenye pendo letu."**

Pili wengi walishangazwa na kuchanganywa na ripoti ya mauaji yake kutoka kwa madaktari ambao awali walidai kuwa alianguka kwenye mmoja wa mifereji ya barabara za Tabata wakati akifanya mazoezi alfajiri.

Pamoja na kwamba ilijulikana kwa wakazi wengi kuwa alikuwa akikimbia kila siku alfajiri lakini ndugu, jamaa, marafiki na hata wananchi hakukuikubali ripoti ya uchunguzi wa madaktari na kusema kuna namna.

Baadhi waliona ajabu ilipotoka ya pili, ikisema kuwa mchumba wake ndiyo walimuua kutokana na wivu wa kimapenzi.

Hii iliwaridhisha na kuwafanya wengi waamini, lakini wale ambao akili yao ilijiongeza walishindwa kukubaliana na ukweli huo.

Kwa nini awali ilisema ameanguka wenyewe kwa ajili ya kupawa na presha ya ghafla alipokuwa anakimbia? Kwa nini safari hii ije tena ripoti ya pili kusema ni mchumba wake? Waliojiongeza walijua kabisa kuwa ameangushiwa jumba bovu. Wakajua yoyote aliye nyuma ya mpango huu, basi ndiye aliyemsingiliza Kamal. Lakini halishindwa kusema popote kwa sababu Jeshi la Polisi ndilo lililotoa taarifa hiyo.

Sasa mambo yote yalikuwa mahakamani. Walisomewa mashtaka ambayo wote waliyakana, lakini walilazimika kukaa rumande. Hii ilisababisha mtuhumiwa namba moja Materu kukatwa jina lake kwenye kinyang'anyiro cha kuwania ubunge.

Ushahidi wa kesi hiyo ulipoanza watu walizidi kumiminika Mahakama Kuu ambapo afande Willy na aliyetajwa awali kama mtuhumiwa Kamal walianza kutoa ushahidi wa kile walichokusanya kwenye upelelezi wao hadi kumgundua Materu ambaye ni bosi wake na wenzake wanane kuwa alihusika.

Kamal ndiye aliyeanza kwa kudai alianza kupokea vitisho kutoka kwa watu ambao hakuwajua kuwa amuache mwanamke aliyenaye kwa sababu si saizi yake.

Aliwasilisha ushahidi wa simu yake ya mkononi ambayo ilikuwa na meseji kadhaa ambazo zilipokelewa kama kielelezo mahakamani.

"Nakumbuka nilishawahi kuandikiwa meseji kibao za vitisho na watu hao ili nimuache mchumba wangu.

Vitisho vilikuwa vikubwa, wengine wakisema wataniwekea sumu kwenye chakula, vinywaji, mara watanikodishia majambazi, kunigonga na gari, baadhi walitishia hata kuniendea kwa waganga wa kienyeji." Kamal alitoa ushahidi wake mahakamani.

"Haiwezekani wewe kapuku tu ukawa na mtoto mzuri kama yule, tunamuomba jiondoe kabisa, muache ili wakubwa tule raha. Ukibisha tutajua la kukufanya, maiti yako haitapelekwa kwa ndugu zako, tutawapeleka samaki baharini, au ndege au wanyama porini." Hiyo ilikuwa ni moja ya meseji ambayo aliitoa kama kielelezo.

"Nikaogopa, nikakata tamaa nikaenda kuaazimia kumuacha. Siku moja nikamwita nyumbani kwangu na kumwambia kama maneno haya, ambayo nakumbuka niliyarekodi kwenye simu yake ya mkononi.

Akatoa simu yake na kibonyeza kitufe na maneno ikasikika sauti yake siku ambayo aliongea na mpenzi wake jinsi alivyopokea vitisho kwa watu asiowajua.

"Mariamu mchumba wangu, nyota nadhifu wa moyo wangu, naomba unikubalie hili nitakalokuomba, kama ulivyonikubalia tukawa sote.

Kwa sasa najijutia mpenzi, nimejitosa ndani ya moto na matatizo, kuwa na wewe imekuwa nongwa, kwao ni kero kwa wasiopenda niwe na wewe."

Mariamu, wewe ni mrembo, Mungu hakukubakisha kitu, ni mzuri, mrembo una umbile zuri, lakini uzuri wako na ufukara kwao ni vibaya, roho zinawauma."

Ninachokuomba sasa Mariamu, imenibidi, ni bora nilivue mimi hili penzi, niwape nafasi waoamini umeshushwa kwa ajili yao si vyema uwe na mimi."

"Ingawa tumeapa kutotengena nawe mpaka kifo kabla hata hatujafunga ndoa, lakini inatubidi tutengane, niwaridhishe wale wabaya kwenye pendo letu."

Klipu ilimalizika na kuanza kuwaliza akinamama wengi mahakamani hapo baada ya kuisikia.

Kuwabembeleza haikuwezekana, badala yake majaji waliamua waiahirishe kesi hiyo hadi siku nyingine.

Maneno hayo ndiyo yaliyochukua kichwa vya habari kesho yake kwenye magazeti na kutamkwa kwenye televisheni na mitandao ya kijamii.

Yaliendelea kuwahuzunisha wengi kuona kumbe hata kabla Mariamu hajauawa mpenzi wake alipata vitisho vilivyomfanya atake kumuacha. Sasa kwa nini hakumuacha? Kwa nini aliendelea naye? Kwa nini badala ya kuuawa mwanaume, akauawa Mariamu? Hilo lingejulikana kama kusingekuwa na vilio mahakamani kiasi cha majaji kuahirisha kesi hiyo yenye mvuto.

***Itaendelea Jumamosi***

## New City yatamba itafanya makubwa

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

TIMU ya New City FC imesema bado wana muda wa kurekebisha makosa yao na kuanza kufanya vizuri katika michezo ya Ligi Kuu Zanzibar inayoendelea, imeelezwa.
New City FC imepata ushindi wa kwanza katika ligi hiyo baada ya kuwafunga Inter Zanzibar mabao 2-1 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa nje wa Amaan (Annex B) juzi.
Tayari New City imecheza michezo nane ya Ligi Kuu Zanzibar, imeshinda mechi moja, imetoka sare mara mbili na imefungwa michezo mitano.
Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa New City, Razak Rajab, alisema jana licha ya timu yake kupata matokeo mabaya mfululizo katika ligi hiyo, lakini wanaimani watazinduka na kufanya vizuri kwenye michezo inayokuja.
Rajab alisema hawalaumu wachezaji kwa matokeo mabaya ya michezo iliyotangulia na kuongeza kufungwa ni sehemu ya ‚maisha' ya soka.
„Tutaimarika, tunaendelea kujipanga, siwezi kuwalaumu wachezaji wangu kwa kufanya vibaya katika michezo iliyotangulia, tunaelewa upepo mbaya wa matokeo ulituangukia, ni jambo la kawaida hasa katika mchezo huu wa soka," Rajab alisema.
Aliongeza hakuna timu ambayo inafanya usajili mbaya au inajiandaa kufungwa, na kinachotokea ni kushindwa kupata matokeo mazuri.
„Ligi ni ngumu na inaushindani mkubwa, ndio maana hatuwatupii lawama wachezaji wetu wala hatulalamikii usajili tuliofanya, tunaendelea kufanyia kazi makosa tunayoyabaini na kujipanga na michezo iliyoko mbele.
Bado tunamatumaini ya timu kubadilika na kufanya vizuri katika ligi hii inayoendelea, bado nafasi tunayo ya kufanya hivyo ndio kwanza tupo kwenye mzunguko wa kwanza, mpira ni mchezo wa kushangaza na tutawashangaza," alisema kocha huyo.
Hata hivyo amewapongeza mashabiki wao wachache wanavyoendelea kuwapa hamasa katika michezo yote wanayoshuka uwanjani bila kuangalia matokeo wanayoyapata.
"Tunamashabiki ambao wana mioyo ya kipekee kabisa, wanaumia na timu yao lakini hawachoki kuja kutuhamasisha kila mchezo, hawaangalii michezo iliyopita ilivyotokaje, ingawa wapo waliopoteza matumaini, tunaahidi tutaendelea kupambana kwa ajili yao," aliongeza.
Katika msimamo wa ligi hiyo inayotoa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, New City yenye pointi tano iko kwenye nafasi ya 12.

# WANARIADHA 50 KUCHUANA LADIES FIRST ZANZIBAR 2024

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

WANARIADHA 50 kutoka mikoa mitano ya visiwani hapa wanatarajiwa kushiriki katika mashindano ya 'Ladies First' yatakayofanyika kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, imeelezwa.

Wanariadha hao watachuana katika hatua ya awali ya kupata wawakilishi wa tano wa kila mkoa.

Nyota watakaopatikana wataungana na wawakilishi wengine wa mikoa 26 ya Tanzania Bara ili baadaye watachuana kwenye ngazi ya taifa itakayofanyika Novemba 23 na 24, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na wanahabari jana, Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BMTZ), Said Kassim Marine, alisema katika hatua ya awali kila mkoa utawakilishwa na wasichana 10.

Marine alisema mashindano hayo yatashirikisha wasichana wenye umri chini ya miaka 20.

Alisema mashindano hayo kwa hapa Zanzibar ni ya kwanza kufanyika hivyo anaamini itakuwa ni fursa nzuri kwa wanariadha wasichana kutangaza vipaji vyao.

Aliongeza kwa upande wa Zanzibar mashindano hayo yatafanyika chini ya udhamini wa Shirika la UN Women na watajipanga kuhakikisha malengo ya michuano hiyo yanafikiwa kikamilifu.

„Maandalizi kwa ajili ya mashindano haya yako katika hatua za mwisho, tunaamini wanariadha wote wanaotarajia kupeperusha bendera za mikoa yao wanaendelea kujiimarisha, tunaamini yatakuwa na ushindani kwa sababu Zanzibar ina vipaji," Marine alisema.

Naye mwanzilishi wa mashindano hayo mwanariadha wa zamani, Juma Ikangaa, alisema lengo kuu la wazo la kuanzishwa mashindano hayo ni kuziba pengo la ushiriki wa wanawake katika michezo na kuwapa fursa vijana kuonyesha ushindani.

Ikangaa alisema wanatarajia kuona viwango vya juu katika mashindano hayo ambayo pia yatawasaidia wasichana kujiandaa vizuri katika michuano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa.

Mwakilishi wa Shirika la Maendeleo la Watu wa Japan (JICA), Hitoshi Ara, alisema mashindano hayo yatatoa fursa kwa wasichana kufanya vizuri katika mashindano ya kanda hapo baadaye.

Ara alisema madhumuni makubwa ya mashindano hayo ni kuwapa thamani wanawake kushiriki katika michezo hasa kupitia mashindano haya ya riadha.

Alisema kufanyika mashindano hayo Zanzibar ni mwanzo mpya wa kuwainua wanawake kupitia riadha.

"JICA itaendelea kusaidiana na serikali katika miradi mbalimbali ya kimaendeleo ikiwamo michezo," Ara alisisitiza.

Mashindano hayo la Ladies First ni ya sita kufanyika mwaka huu ambapo mara ya kwanza ilikuwa mwaka 2017 na JICA walikuwa wadhamini kupitia wazo lililotolewa na Ikangaa ambaye ni balozi wa hiari wa shirika hilo.



Wachezaji wa Coastal Union wakifanya mazoezi kujiandaa kuikaribisha Yanga katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha. **PICHA: MTANDAO**

# Balua aipania JKT Tanzania

Na Shufaa Lyimo

WINGA wa Simba, Edwin Balua, amesema baada ya kupata ushindi dhidi ya Prisons, sasa wachezaji wamejipanga kuhakikisha wanaondoka na pointi nyingine tatu watakapokutana na JKT Tanzania katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa Oktoba 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Balua, alisema malengo yao ni kujituma na kucheza katika kiwango cha juu ili kupata ushindi na kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Balua alisema wataikaribisha JKT Tanzania kwa nidhamu kwa sababu wanafahamu ni timu yenye wachezaji wazoefu.

"Malengo yetu ni kupata ushindi katika mchezo wetu ujao ambao tutakuwa kwenye uwanja wetu wa nyumbani, tumejiandaa kukutana na upinzani," alisema Balua.

Aliongeza kila mchezaji wa Simba yuko tayari kupambana kwa sababu hawataki kuona wanapoteza tena pointi.

Nyota huyo pia aliwashukuru mashabiki pamoja na wanachama wa klabu hiyo kwa kuendeleza ushirikiano katika kila mechi wanayocheza na hali hiyo inawaongezea nguvu ya kufanya vizuri.

"Tunawashukuru mashabiki wetu kwa ushirikiano na sapoti wanayotupa kwa sababu tunaamini bila mashabiki hatuwezi kufanya lolote," Balua alisema.

Aliongeza msimu huu ni mgumu kwa sababu kila timu imefanya usajili mzuri na hatuna inayokubali kupoteza mchezo wake kirahisi.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CITY KUMUUZA WALKER

KLABU ya Manchester City iko tayari kumuuza nahodha, Kyle Walker, mwenye umri wa miaka 34, kwa takriban pauni milioni 15 msimu ujao wa joto. Beki huyo wa England analengwa na Al-Ahli ya Saudi Arabia. ***(Daily Star)***

### CITY, LIVERPOOL VITANI

MANCHESTER City na Liverpool zimeonyesha nia ya kumnunua mshambuliaji wa Brighton raia wa Argentina, Facundo Buonanotte, mwenye umri wa miaka 19, ambaye yuko kwa mkopo Leicester City. ***(Fichajes)***

### KERKEZ APANDISHWA DAU

KLABU ya Bournemouth itataka „fedha nyingi" kama watamuuza beki wa Timu ya Taifa ya Hungary, Milos Kerkez, mwenye umri wa miaka 20, ambaye anazivutia Liverpool, Arsenal na Manchester United. ***(Football Insider)***

### MRITHI WA VAN DIJK ASAKWA

LIVERPOOL inamlenga beki wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Nico Schlotterbeck, mwenye umri wa miaka 24, kama mbadala wa Virgil van Dijk, iwapo Mholanzi huyo ataondoka katika klabu hiyo msimu ujao wa joto. ***(Caught Offside)***

### SEMENYO: NAIPENDA ARSENAL

ARSENAL imetiwa moyo iwapo inataka kumnunua mshambuliaji wa Bournemouth, Antoine Semenyo, mwenye umri wa miaka 24, baada ya kusema yeye ni shabiki wa washikabunduki hao na anataka kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Football 365)***

### FERMAMDEZ ANUKIA UNITED

KLABU ya Manchester United huenda ikamsajili tena beki wa kushoto, Alvaro Fernandez, mwenye umri wa miaka 21, ambaye alijiunga na Benfica kwa mkataba wa kudumu msimu wa joto na anafuatiliwa na Liverpool na Real Madrid. ***(Teamtalk)***

### BARCA KUMBAKISHA ARAUJO

BARCELONA imeanzisha mazungumzo ya kuhusu makubaliano ya mkataba mpya kwa mlinzi, Ronald Araujo, mwenye umri wa miaka 25 anayelengwa na Manchester United na Chelsea, na kiungo, Frenkie de Jong (27), ambaye pia anasakwa na Mashetani Wekundu. ***(90 min)***

### POGBA MAMBO MAGUMU

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Paul Pogba, mwenye umri wa miaka 31, anaonekana kutokuwa na uwezekano wa kuichezea tena Juventus mara tu marufuku yake ya kutumia dawa za kusisimua misuli itakapokamilika Machi, mwakani baada ya mkurugenzi wa klabu hiyo kusema kikosi kimekamilika bila yeye. ***(DAZN, via ESPN)***

### TUCHEL ANUKIA NEEMA

KOCHA mpya wa England, Thomas Tuchel atapokea marupurupu ya pauni milioni tatu endapo atafanikisha kuiongoza timu hiyo kushinda ubingwa wa Kombe la Dunia la 2026. ***(The Sun)***

### GUEHI ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United iko tayari kufufua mpango wa kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya England na Crystal Palace, Marc Guehi, mwenye umri wa miaka 24 katika dirisha la Januari kwa ada ya takriban pauni milioni 80. ***(Team Talk)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ONANA: WACHEZAJI MAN UNITED HAWANA FURAHA

●●●Kipa huyo afunguka licha ya kupata sare, lakini walikuwa bora...

**MANCHESTER, England**

MLINDA mlango wa Manchester United, André Onana, ametaja sare yao ya bao 1-1 dhidi ya Fenerbahce katika mechi ya Ligi ya Europa ni ya „kukatisha tamaa".

United walitangulia kupitia kwa Christian Eriksen kabla ya Youssef En-Nesyri kusawazisha punde tu baada ya kipindi cha mapumziko.

Onana alicheza jukumu lake katika kupata pointi kwa United kwa kuokoa mara mbili mashuti ya En-Nesyri, lakini baadaye kipa huyo alisisitiza chumba cha kubadilishia nguo „hakikuwa na furaha."

"Ni huzuni kubwa kwangu na kwa mashabiki wa klabu, kama mchezaji wa Manchester United una wajibu wa kujaribu kushinda," alisema Onana akiiambia TNT Sports.

"Hatukushinda, lakini angalau hatujapoteza, sio furaha bila shaka, lakini tunaendelea kuchukua jukumu na kwenda tena.

Tuliruhusu bao la mapema katika kipindi cha pili, tulipaswa kuonyesha tabia na nadhani ndivyo tulivyofanya. Hatukushinda lakini nilifikiri tulikuwa bora kuliko wao."

Katika usiku huo huko Istanbul, Kocha wa Fenerbahce, Jose Mourinho, alitolewa kwa kadi nyekundu kwa kumlalamikia mwamuzi.

# Mancini aachia ngazi Saudia

**RIYADH, Saudi Arabia**



ROBERTO Mancini ameacha nafasi yake kama kocha mkuu wa Timu ya Taifa ya Saudi Arabia, shirikisho soka la nchi hiyo limesema.

Mancini, ambaye alishinda ubingwa wa Ulaya akiwa na kikosi cha Italia mwaka 2021, ameondoka kwa makubaliano ya pande zote, shirikisho hilo lilisema.

„Bodi ya Wakurugenzi ya Shirikisho la Soka la Saudia na kocha wa timu ya taifa, Roberto Mancini, imefikia makubaliano ya pamoja siku ya Alhamisi kumaliza uhusiano wa kimkataba," timu ya taifa ilichapisha kwenye mtandao wa kijamii wa X.

Kocha huyo wa zamani wa Inter Milan na Manchester City alishinda mataji mengi katika maisha ya soka kama mchezaji na kocha.

Lakini alishindwa kuiongoza Saudi Arabia kushinda Kombe la Asia mwaka huu, akiondolewa katika michuano hiyo katika hatua ya 16 bora.

Vitendo vyake wakati wa mechi hiyo nchini Qatar pia vilizua utata alipotoka kabla ya kumalizika kwa timu yake kupoteza kwa penalti dhidi ya Korea Kusini. Baadaye aliomba msamaha.

Mancini alikuwa ameajiriwa na Saudi Arabia tangu Agosti mwaka jana, wiki mbili baada ya kuacha kazi yake ya kuiongoza Italia.

Saudia wamo katika nafasi ya tatu katika Kundi C la Asia katika hatua ya tatu ya mchujo wa Kombe la Dunia wakiwa na pointi tano.

Wameachwa kwa pointi tano na vinara wa kundi hilo, Japan baada ya kucheza mechi nne.

Walifungwa mabao 2-0 nyumbani na Japan Oktoba 10, mwaka huu kabla ya kulazimishwa sare ya bila kufungana na Bahrain siku tano baadaye.

Timu mbili za juu katika kila kundi zinafuzu moja kwa moja katika fainali za Kombe la Dunia huku timu zilizoshika nafasi ya tatu na nne zikiingia katika hatua nyingine ya mchujo huku zile mbili za mwisho zikitolewa.

# Courtois kuikosa Clásico

**MADRID, Hispania**




GOLIKIPA, Thibaut Courtois ataikosa mechi ya El Clásico ya wikendi hii dhidi ya Barcelona kutokana na jeraha la mguu wake wa kushoto ambalo linaweza kumweka nje kwa wiki tatu hadi nne, vyanzo viliiambia ESPN.

Kipa huyo wa Real Madrid hapo awali alipata jeraha wakati wa sare ya bao 1-1 na Atlético Madrid Septemba 29, mwaka huu.

Baada ya wiki mbili za kuwa nje, Courtois alichangia katika ushindi dhidi ya Celta Vigo na Borussia Dortmund, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 alipata jeraha katika mchezo huo.

„Kufuatia vipimo vilivyofanywa kwa mchezaji wetu, Thibaut Courtois na huduma za matibabu za Real Madrid, amegundulika kuwa na jeraha katika mguu wake wa kushoto," klabu hiyo ilisema katika taarifa yake.

Vyanzo vimeiambia ESPN Courtois atakosa mechi ya Clasico na pia michezo dhidi ya Valencia na AC Milan.

Inaonekana kuna uwezekano mkubwa ataweza kurejea katika utimamu wake kucheza dhidi ya Osasuna, ingawa hiyo itategemea kasi ya kupona kwake.

Vyanzo vya klabu viliiambia ESPN wana ufahamu mzuri wa aina hii ya jeraha baada ya kulishughulikia mara mbili msimu uliopita.



# FLICK APONGEZWA KUWAJENGA CHIPUKIZI

**BARCELONA, Hispania**

KIUNGO wa kati wa Barcelona, Pedri amemsifu kocha wa timu hiyo, Hansi Flick, kwa kuwapa wachezaji wachanga ujasiri unaohitajika ili kuimarika.

Barca wana timu changa zaidi katika LaLiga, wakiwa na wastani wa umri wa miaka 23.6.

Barca wapo mbele kwa pointi tatu dhidi ya Real Madrid kileleni katika msimamo wa ligi hiyo kuelekea mechi ya Clásico itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Bernabéu.

„Ni muhimu sana," alisema Pedri akiiambia ESPN kuhusu kujitolea kwa Flick kukuza vipaji vya wachezaji vijana.

„Ujasiri ambao kocha anawapa wachezaji wachanga wote wanaokuja, wanarudisha shukrani kwa kucheza vizuri. Hii inawawezesha kujiamini, kuwa na uhuru zaidi wa kuthubutu kujaribu mambo."

Flick aliwaanzisha wachezaji sita kutoka akademi ya vijana katika ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Bayern Munich, mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyofanyika Jumatano iliyopita ukiwa ni ushindi wa pili kwa Barca katika mashindano hayo.

„Tunaona wachezaji wengi ambao wanatoka La Masia (akademi ya Barcelona) na ndio roho ya klabu hii," alisema Pedri.

Dani Olmo, ambaye alirejea Barca kutoka Leipzig msimu huu wa joto, ana furaha kuona wachezaji wa akademi wakipata fursa.

Akiwa bidhaa ya vijana wa Barca, Olmo alijiunga na Dinamo Zagreb alipofikisha umri wa miaka 16.

"Inashangaza," Olmo aliiambia ESPN. „Barcelona ni akademi bora zaidi duniani. La Masia wameonyesha hili kwa miaka yote, hivyo tunasherehekea sasa, tukiwa na kikosi cha kwanza wachezaji wengi waliokulia La Masia. Inatoa motisha kwa wachezaji wote."

Kipa mkongwe wa Poland, Wojciech Szczęsny, ambaye alistaafu na kujiunga na Barca mapema mwezi huu kufuatia jeraha la Marc-André ter Stegen, amekiri vijana wengi kwenye timu huchukua muda kuzoea.

„Lazima nikwambie, ni ya kushangaza," aliiambia ESPN. "Baadhi ya wachezaji hawa labda hawajaniona nikiichezea Arsenal na ninahisi kama hiyo haikuwa muda mrefu uliopita! „Lakini ni jambo kubwa kwa nini niliamua kuja kwa sababu nadhani ninaweza kutoa kitu kwa timu hii."

HABARI MICHEZO

# SHIME: TUKO FITI KUIKABILI SUDAN NA KUPATA USHINDI

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Bakari Shime, amesema kikosi chake tayari kimemaliza maandalizi ya kuikabili Sudan katika mchezo wa kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), utakaochezwa kesho nchini Mauritania.

Sudan imepeleka mechi zake Maurtania kutokana na kuwapo kwa machafuko ya vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini mwao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Shime, amesema amekiandaa vyema kikosi hicho kucheza katika mazingira yoyote hasa ikizingatiwa timu zote mbili hazitakuwa nyumbani.

"Maandalizi yote yamekamilika kwa asilimia 99, mbinu tulizoziweka katika mchezo huu naamini zitafanya kazi na tutapata ushindi," alisema Shime.

Kocha huyo alisema hali ya hewa haiwapi shida hata kidogo kwa sababu tofauti ya nchi na nchi katika Bara la Afrika ni ndogo.

"Hali ya hewa kijiografia Afrika inafanana kidogo, sehemu kuna joto sana na sehemu nyingine baridi, kwa hiyo tumejiandaa kucheza katika mazingira yoyote," Shime alisema.

Kuhusu wachezaji wa kikosi hicho ambao wengi wameonekana hawana uzoefu, kocha huyo alisema hata wale wenye uzoefu walianza kama wao na anaamini watafanya vizuri.

"Kwa wachezaji wangu nitapanga kikosi ambacho naona kinaweza kunisaidia kwa wakati ule haijalishi wana uzoefu au hawana, ni tunaposema uzoefu wengi wao ni wa kimafaifa tu, lakini wana uzoefu kwenye klabu zao wanazocheza," aliongeza kocha huyo.

Wachezaji walioitwa katika mechi hiyo, nyota 11 wanatoka kwenye kikosi cha timu ya taifa ya vijana chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), lakini pia yupo kipa mkongwe, Aishi Manula kutoka Simba.

Stars iliwasili salama nchini humo juzi na baadaye mechi ya kesho, itarejea nyumbani kuendelea na maandalizi ya mchezo wa marudiano utakaofanyika Novemba 3, mwaka huu.



Wachezaji wa Dodoma Jiji wakimsikiliza kwa makini kocha wao (hayupo pichani), kwa ajili ya maandalizi ya kuikaribisha JKT Tanzania katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Jamhuri. **PICHA: MTANDAO**

# Simba Queens yaitisha Ceasiaa

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Simba Queens kinaendelea na mazoezi kwa ajili ya kuifuata Ceasiaa katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), itakayochezwa Novemba 5, mwaka huu kwenye Uwanja wa Samora mkoani, Iringa.

Meneja wa Simba Queens, Selemani Makanya, aliliambia gazeti hili wanautumia vyema muda wa mapumziko kurekebisha makosa yao kwa sababu wanahitaji kuendeleza kasi ya ushindi.

Makanya alisema mechi zote za ligi hiyo ni mgumu, hivyo wanajiimarisha katika kila idara kwa sababu hawahitaji kupoteza pointi katika mechi hiyo ya ugenini.

"Tunawajua vizuri Ceasiaa, tunajiimarisha pale ambapo tumeona kuna shida ili tutakaposhuka dimbani tusiwe na hofu, ligi ya wanawake imezidi kupanda, hakuna mechi rahisi, hakuna mpinzani rahisi, mechi zote sawa na fainali," Makanya alisema.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa Novemba 5, mwaka huu ni kati ya Yanga Princess dhidi ya Mashujaa Queens wakati JKT Queens itawakaribisha Mlandizi Queens kutoka Pwani na Gets Program itawakabili Bunda Queens ya Mara.

Fountain Gate Princess ya Dodoma itakuwa mwenyeji wa Alliance Girls kutoka jijini Mwanza.

Bingwa wa ligi hiyo hupata nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

# Raizin kinara mabao Ligi ya Championship

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa Coastal Union na Dodoma Jiji, Raizin Hafidh, anaongoza kwa kupachika mabao katika Ligi ya Championship, akifikisha magoli matano, katika michezo mitano ambayo timu yake ya Mtibwa Sugar imecheza.

Raizin, ambaye hivi karibuni aliteuliwa kuwa mchezaji bora wa ligi hiyo wa Septemba, wiki hii alifunga bao la kusawazisha katika mchezo ambao Mtibwa Sugar ilitoka sare ya 1-1 dhidi ya wenyeji Polisi Tanzania.

Straika huyo ambaye kipaji chake kilionekana akiwa na Coastal Union, alifunga bao kwa penalti dakika ya 38 lililowaokoa Mtibwa Sugar kupata kipigo kutoka kwa Polisi Tanzania.

Nyota huyo msimu huu kwa kufunga mabao yote mawili dakika ya 35 na 70 katika mchezo wa kwanza ambapo walicheza dhidi ya Green Warriors kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro.

Katika mechi iliyofuata Mtibwa ikiwa ugenini dhidi ya Cosmopolitan, alifunga bao moja kwenye ushindi wa magoli 2-0, moja likifungwa na Omari Marungu ambaye alipandishwa kwenye kikosi cha kwanza kutoka timu ya vijana wa umri chini ya miaka 20.

Alipachika tena bao moja katika mchezo mwingine ambao Mtibwa iliwaalika Mbeya City na kuwafunga mabao 2-0, moja likitiwa kwenye kamba na beki wa zamani wa Kagera Sugar, Erick Kyaruzi.

Mabao yake matano mpaka sasa akiwa kinara wa mabao, pia yanaifanya Mtibwa Sugar kuongoza ligi hiyo, ikiwa na pointi 13 kwa michezo mitano iliyocheza, ikishinda minne na sare moja.

Nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo yenye timu 16 inashikiliwa na Stand United ya Shinyanga yenye pointi 12, wakati Geita Gold yenye pointi 11 sawa na TMA zinafuatia, lakini kabla ya mechi za jana.

Ligi hiyo itaendelea tena kesho kwa Stand United kuikaribisha Mbeya Kwanza wakati Songea United itawaalika TMA na Cosmopolitan itawafuata Kiluvya kwenye Uwanja wa Mabatini ulioko Mlandizi mkoani, Pwani.

Timu mbili zitakazofanya vizuri katika ligi hiyo zitapanda daraja moja kwa moja kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Michezo
Jumamosi Oktoba 26, 2024
Nipashe

Onana: Wachezaji Man United hawana furaha
UKURASA 21



# Simba yaendeleza dozi

Singida Black Stars nayo yajiimarisha kileleni Ligi Kuu Bara baada...




Beki wa Simba, Shomary Kapombe (aliyeruka juu), akishangilia baada ya kufunga bao la kwanza katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana. Kushoto ni Awesu Awesu na Steven Mukwala. Simba ilishinda mabao 3-0. **PICHA: SIMBA SC**

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili ya wachezaji wa kigeni, Jean Charles Ahoua raia wa Ivory Coast, Debora Fernandes Mavambo mwenye uraia pacha wa Angola na Congo Brazaville na Mtanzania Shomari Kapombe yalipa Simba ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Namungo FC , ukiwa ni wa pili mfululizo baada ya kupoteza kwa bao 1-0 dhidi ya watani zao, Yanga.

Simba ambayo Jumanne iliyopita ilipata ushindi wa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Sokoine, Mbeya, ilipata ushindi huo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana na kumaliza mdudu wa sare wa msimu uliopita ilipocheza na timu hiyo.

Novemba 9, mwaka jana katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Simba ililazimishwa sare ya bao 1-1, kabla ya kupata sare ya mabao 2-2 katika mchezo wa mzunguko wa pili uliochezwa ugenini Ruangwa mkoani, Lindi.

Ushindi huo unaifanya Simba kufikisha pointi 19 na mabao 16 ya kufunga katika michezo minane ambayo imecheza mpaka sasa, ikikwea hadi nafasi ya pili.

Simba ilianza kupiga hodi katika lango la wapinzani wao dakika ya pili baada ya Kapombe kukokota mpira kwenye wingi ya kulia na kupiga krosi iliyounganishwa kichwa na Steven Mukwala, lakini ukapaa juu ya lango.

Dakika mbili baadaye ilikuwa ni kama mabadilishano, Mukwala baada ya kupata pasi mpenyezo kutoka kwa Joshua Mutale, aliachia shuti kali lililoonekana linakwenda wavuni, lakini mpira uligonga nguzo ya pembeni chini na ukarejea uwanjani, Kapombe akiwa katika kasi aliuwahi mpira huo na kupiga shuti dhaifu lakini kwa kiufundi lililowapoteza maboya wachezaji nyota watatu wa Namungo pamoja na kipa wao, Jonathan Nahimana, na ukatinga wavuni.

Namungo ilifika langoni mwa Simba kwa mara ya kwanza dakika ya 20, wakati krosi ya Jacob Massawe ilipoleta kizaazaa langoni, lakini ikakosa muunganishaji, dakika moja baadaye ilipata tena nafasi, lakini Paul Buswita alipiga shuti dhaifu ambalo halikumbabaisha kipa wa Mnyama, Moussa Camara.

Mukwala kwa mara nyingine tena, alipaza mpira wa kichwa juu, akiwa amemiminiwa majaro na Awesu Awesu dakika ya 28.

Dakika ya 31, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davis, alilazimika kufanya mabadiliko ya lazima kwa kumtoa Awesu ambaye aliumia na nafasi yake kuchukuliwa na Ahoua, ambaye ilimchukua dakika mbili tu kupachika bao la pili katika mchezo huo.

Alikuwa ni Mukwala tena, akiwa kwenye wingi ya kulia, alipiga krosi iliyomkuta mfungaji aliyepachika bao kwa utulivu mkubwa huku Nahimana akiruka bila mafanikio.

Bao hilo linamfanya kiungo huyo kufikisha mabao matatu msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara huku pia akiwa na ‚asisti‘ nne.

Nusura Namungo ipate bao dakika ya 38, pale, Hassan Kabunda, alipowahadaa mabeki wa Simba na kupiga shuti hatari la chinichini ambalo lilikuwa linaelekea wavuni, kama si jitihada za Camara kuukamata karibu na mstari wa goli.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko ambayo yalisaidia kuongeza mashambulizi, lakini ilikuwa ni Simba ambayo ilifaidika na mabadiliko hayo.

Dakika sita kabla ya mechi kumalizika, Mavambo alipachika bao la tatu, akimalizia pasi mpenyezo kutoka kwa Ateba.

Kipigo hicho kinaiacha Namungo katika nafasi ya 13 ikiwa na pointi sita baada ya kucheza michezo saba.

Mechi ya mapema iliyochezwa kwenye Uwanja wa Liti Singida, wenyeji Singida Black Stars walizidi kujichimbia kileleni, walipoitwanga Fountain Gate mabao 2-0, wakifikisha pointi 22 kwa michezo minane waliyocheza.

Mabao ya Singida Black Stars katika mechi hiyo yalifungwa na Josephat Bada dakika ya 54 na Ayoub Lyanga, dakika ya 65 ya mchezo, huku Fountain Gate ikisalia na pointi zake 16.

## Yanga yaitangazia Coastal Union vita

**Na Adam Fungamwango**

TUTAINGIA kivingine, hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya wenyeji Coastal Union ‚Wagosi wa Kaya‘ itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Coastal Union imepeleka mechi zake za nyumbani Arusha kwa sababu CCM Mkwakwani unaendelea na maboresho mbalimbali.

Gamondi amesema timu yake itaingia katika mechi hiyo tofauti na mashabiki walivyozoea kwa sababu hawataki kudondosha pointi hata moja.

Kocha huyo alisema wameamua kubadilika ‚kidogo‘ kutokana na aina ya uwanja ambao watautumia katika mchezo wa leo ili wasipoteze malengo yao.

“Ratiba imebana ila hatuwezi kulalamika, najua itakuwa mechi ngumu ukizingatia uwanja tutakaochezea si mzuri kwa aina yetu ya soka tunalocheza, tutajaribu kila tunachoweza, tutabadilika kutokana na uwanja ulivyo, lakini siwezi kuwaambia tutachezaje, kwangu mimi siamini sana kwenye mfumo bali ni kwa jinsi gani unatumia nafasi zinazopatikana uwanjani,“ alisema Gamondi.

Aliongeza anatarajia kutumia kikosi kilekile, huku akishangaa baadhi ya watu wakiwamo mashabiki na wachambuzi kumpangia nani acheze na nani asicheze wakati jukumu hilo ni lake yeye kama mwalimu.

“Kupanga wachezaji huo ni uamuzi wangu, timu si inafanya vyema? Kwa nini nibadilishe kikosi, au kulazimisha wachezaji fulani wacheze? Kwa nini mnataka nibadilishe, kwa nini mnataka wachezaji wote wacheze? Mimi ndiyo naamua,“ Gamondi alisema.

Naye Kocha wa Coastal Union, Juma Mwambusi, aliliambia gazeti hili vijana wake wamemwahidi watamkaribisha vizuri kwa kupata ushindi dhidi ya Yanga.

“Nimepata mapokezi mazuri, nimekuja hapa kuhakikisha kile ambacho Coastal Union wanachokihitaji, wanafanikiwa kukipata. Tunajua ni mechi ngumu, tunacheza na mabingwa, hilo nalitambua, wachezaji wangu wamenihakikishia watafanya kila wanaloweza ili wanikaribishe vizuri,“ Mwambusi alisema.

Coastal Union itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya JKT Tanzania wakati Yanga haijapoteza mechi wala kuruhusu nyavu zao kutikiswa msimu huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >